JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA (ACSEE), 2023

## KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA (ACSEE), 2023

# 121 KISWAHILI

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

DIBAJI ........ iv
1.0 UTANGULIZI ........ 1
2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI ........ 2
2.1 SEHEMU YA I: KISWAHILI KARATASI YA KWANZA ........ 2
2.1.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI ........ 2
2.1.1.1 Swali la 1: Ufahamu ........ 2
2.1.1.2 Swali la 2: Matumizi ya Sarufi ........ 8
2.1.1.3 Swali la 3: Matumizi ya Sarufi ........ 14
2.1.1.4 Swali la 4: Utumizi wa Lugha ........ 17
2.1.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAREFU ........ 23
2.1.2.1 Swali la 5: Uandishi wa Insha ........ 23
2.1.2.2 Swali la 6: Tafsiri na Ukalimani ........ 29
2.1.2.3 Swali la 7: Kukua na Kuenea kwa Kiswahili ........ 35
2.1.2.4 Swali la 8: Kukua na Kuenea kwa Kiswahili ........ 42
2.2 SEHEMU YA II: KISWAHILI KARATASI YA PILI ........ 49
2.2.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI ........ 49
2.2.1.1 Swali la 1: Maendeleo ya Fasihi Simulizi ........ 49
2.2.1.2 Swali la 2: Fasihi kwa Ujumla ........ 54
2.2.1.3 Swali la 3: Fasihi kwa Ujumla ........ 57
2.2.1.4 Swali la 4: Usanifu wa Maandishi ........ 62
2.2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAREFU ........ 66
2.2.2.1 Swali la 5: Uhakiki wa Ushairi ........ 66
2.2.2.2 Swali la 6: Uhakiki wa Ushairi ........ 72
2.2.2.3 Swali la 7: Uhakiki wa Riwaya ........ 79
2.2.2.4 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya ........ 86
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA MADA ........ 93
4.0 HITIMISHO ........ 94
5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ........ 94
Kiambatisho A ........ 95
UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2023 ........ 95
Kiambatisho B ........ 96
ULINGANIFU WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MWAKA 2022 NA 2023 ........ 96

# DIBAJI

Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa katika Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita mwaka 2023 imeandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania ili kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakuza mitaala na wadau mbalimbali wa elimu kuhusu matokeo ya watahiniwa katika somo la Kiswahili kwa ujumla.

Taarifa hii ni tathmini ya mwisho inayolenga kuonesha mafanikio ya mfumo wa elimu katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa watahiniwa wa Kidato cha Sita. Kimsingi uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani huu unalenga kuonesha dhahiri maarifa ambayo mfumo wa elimu uliweza au haukuweza kuwapa watahiniwa katika somo la Kiswahili kwa kiwango cha Sekondari, Kidato cha Tano hadi cha Sita.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuonesha sababu za watahiniwa kufanya vizuri, vibaya, au kwa kiwango cha wastani katika maswali/mada mbalimbali zilizopimwa. Ripoti hii inaonesha baadhi ya sababu zilizofanya watahiniwa kufanya vizuri kama vile kuwa na uelewa mzuri wa mada na uzingatiaji mkubwa wa matakwa ya swali. Pia, sababu za watahiniwa kuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu zimeelezwa kuwa ni pamoja na kutoa majibu yasiyojitosheza. Aidha, sababu zilizofanya watahiniwa wachache kupata alama hafifu katika majibu yao zimefafanuliwa kama vile kutoelewa matakwa ya swali, uwezo mdogo wa kuelezea dhana mbalimbali kwa ufasaha, udhaifu katika kutathmini maandishi ya kisanaa, na kutokuelewa dhana mahsusi zinazohusiana na somo la Kiswahili kwa ujumla.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau wote wa elimu kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ili kuondoa changamoto chache zilizobainishwa katika taarifa hii. Vilevile, Baraza linaamini kuwa kiwango cha ufaulu katika somo hili kitaendelea kuwa bora zaidi iwapo mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa hii yatazingatiwa ipasavyo.

Mwisho, Baraza linatoa shukurani za dhati kwa wote walioshiriki katika mchakato wa uandishi wa taarifa hii.

Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita uliofanyika mwezi Mei 2023 uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo la Kiswahili Kidato cha Tano na Sita. Mtihani wa somo la Kiswahili ulikuwa na karatasi mbili ambazo ni 121/1 Kiswahili 1 iliyotahini mada za *Ufahamu na Ufupisho*, *Utumizi wa Lugha*, *Matumizi ya Sarufi*, *Utungaji*, *Maendeleo ya Kiswahili*, na *Tafsiri na Ukalimani*; na 121/2 Kiswahili 2 ambayo ilitahini mada za *Fasihi kwa Ujumla*, *Maendeleo ya Fasihi Simulizi*, *Usanifu wa Maandishi*, na *Uhakiki wa kazi za Fasihi Andishi*.

Mtihani wa 121/1 Kiswahili 1 ulikuwa na sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali manne (4) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu B ilikuwa na maswali manne (4). Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu ambapo, swali la sita (6) lilikuwa la lazima.

Mtihani wa 121/2 Kiswahili 2 ulikuwa na sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali manne (4) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu B ilikuwa na maswali manne (4). Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu (3) ambapo, swali la sita (6) lilikuwa la lazima.

Jumla ya watahiniwa 29,184 walifanya mtihani wa Kiswahili ambapo wavulana walikuwa 14,657 na wasichana walikuwa 14,527. Takwimu zinaonesha kuwa somo hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa kati yao, watahiniwa 29,183 walifaulu kwa kupata daraja A hadi S na mtahiniwa mmoja (1) alipata alama chini ya 35 (daraja F). Jedwali Na. 1 linaonesha ulinganifu wa ufaulu wa watahiniwa kwa kila daraja kwa mwaka 2022 na 2023.

**Jedwali Na. 1: Ufaulu wa Watahiniwa kwa kila Daraja**

| **Mwaka** | **Waliofanya** | Ufaulu (%) | **Gredi za Ufaulu** (%) | | | | | | **Walifeli** (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **A** | **B** | **C** | **D** | **E** | **S** | **F** |
| 2021 | 20,756 | 100 | 0.78 | 33.24 | 55.42 | 10.02 | 0.53 | 0.02 | 0 |
| 2022 | 24,944 | 100 | 1.59 | 44.42 | 49.38 | 4.47 | 0.13 | 0.01 | 0 |
| 2023 | 29,184 | 100 | 3.65 | 39.71 | 47.65 | 8.28 | 0.44 | 0.01 | 0 |

Katika **Jedwali Na. 1**, takwimu zinaonesha kuwa asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika madaraja kwa mwaka 2023 iliongezeka katika daraja A, D na E, na ilipungua katika daraja B na C pekee. Hata hivyo, ufaulu wa watahiniwa kwa

mwaka 2023 ulikuwa mzuri zaidi katika daraja A kwani watahiniwa wengi (1,064) walifaulu. Ufaulu katika daraja hili ni zaidi ya mara mbili ikilinganishwa na mwaka 2022 ambapo watahiniwa 398 pekee ndio waliofaulu katika daraja hilo. Pia, takwimu katika miaka mitatu zinaonesha kuwa watahiniwa wengi walifaulu katika madaraja ya juu (A, B na C) na ufaulu katika madaraja ya chini ulikuwa na watahiniwa wachache.

Uchambuzi umefanyika ili kubainisha jinsi maswali yalivyojibiwa, namna yalivyopaswa kujibiwa na changamoto zilizojitokeza. Uchambuzi umezingatia matokeo ya watahiniwa yaliyowekwa katika viwango vitatu vya ufaulu yaani *vizuri, wastani*, na *hafifu*. Kiwango kizuri cha ufaulu ni alama 60 hadi 100, wastani alama 35 hadi 59 na ufaulu hafifu alama 0 hadi 34. Aidha, chati na majedwali mbalimbali yametumika kufafanua viwango vya ufaulu ambapo katika kila chati au jedwali, rangi nyekundu inawakilisha ufaulu hafifu, njano ufaulu wa wastani, na kijani ufaulu mzuri. Hata hivyo, sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatanishwa katika kila swali ili kudhihirisha maelezo ya uchambuzi.

# 2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI

Uchambuzi wa majibu kwa kila swali umefanyika ili kuonesha ufafanuzi wa kina wa majibu yaliyotolewa na watahiniwa kwa kila swali na kuonesha maswali yaliyofanyika kwa kiwango kizuri, cha wastani, na kiwango hafifu. Vilevile, sababu za ufaulu wa watahiniwa zimeelezwa bayana kwa kila swali.

## 2.1 SEHEMU YA I: KISWAHILI KARATASI YA KWANZA

Karatasi ya kwanza imegawanyika katika sehemu A na B. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ni kama inavyoonekana katika sehemu zifuatazo:

### 2.1.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne (4) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na alama kumi (10).


#### 2.1.1.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali lilitoka katika mada ndogo ya *Ufahamu wa Kusoma na Ufupisho*. Swali hili lilikuwa linapima uelewa wa mtahiniwa katika

kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali yaliyohusiana na habari hiyo. Swali lilikuwa na vipengele vinne, (a) hadi (d).

Swali lilimtaka mtahiniwa (a) kuandika kichwa cha habari kisichozidi maneno matatu; (b) kubainisha sababu mbili zilizowazuia wanafunzi kushiriki mambo ya jadi wakati wa enzi za ukoloni; (c) kufafanua maana ya maneno (i) *Wamisheni*, (ii) *Wahisani*, (iii) *Wamegutuka*, na (iv) *Wazungu weusi* kama yalivyotumika katika habari; na (d) kutumia maneno yasiyopungua ishirini kufafanua wazo kuu la mwandishi lililopo katika aya ya nne.

Swali lilijibiwa na watahiniwa 29,184 sawa na asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri sana kwa kuwa watahiniwa 24,983 sawa na asilimia 85.60 walifaulu kwa kiwango kizuri hadi cha wastani. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na.1:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Katika Chati Na. 1, watahiniwa 4,201 (14.39%) walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 3, watahiniwa 11,616 (39.80%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5 na watahiniwa 13,367 (45.81%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 6 hadi 10.

Ufaulu mzuri wa watahiniwa 13,367 (45.81%) ulitokana na uelewa wa kifungu cha habari na kuweza kutoa majibu sahihi katika vipengele vingi vya swali hili. Watahiniwa hao waliweza kupendekeza kichwa


cha habari kama ELIMU YA KIKOLONI/ATHARI YA ELIMU YA KIKOLONI/CHANGAMOTO ZA ELIMU YA KIKOLONI kwa usahihi. Pia walibainisha kwa usahihi sababu mbili zinazowafanya wanafunzi kuzuiliwa kushiriki katika mambo ya jadi wakati wa enzi ya ukoloni kama vile; *kuwatenga na jamii yao ili iwe rahisi kuwatawala* na *kurahisisha upandikizaji wa jadi za kikoloni*. Vilevile waliweza kufafanua kwa usahihi maana ya kila neno walilopewa kwa kuandika: *wamishenari* ni kundi la watu wanaotangaza dini hasa ya ukristo; *wahisani* ni watu au nchi inayotoa misaada kwa watu/nchi; *wamegutuka* ni kustuka/kung'amua; na *wazungu weusi* kuwa ni waafrika wenye tabia na mienendo ya wazungu. Kadhalika, walifafanua wazo kuu la mwandishi linalopatikana katika aya ya nne kwa maneno yasiyopungua ishirini kwa usahihi kama vile; *wanafunzi kufundishwa sanaa za maonyesho za kizungu, wakazipokea, wakazienzi na kuacha mila na desturi zao njema kwa madai kuwa hazifai.* Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu sahihi katika vipengele (a) hadi (d).


1. a) ATHARI ZA ELIMU YA KIKOLONI.

b) i. Wakoloni waliamini kuwa Sanaa za Maonesho ya jadi ni Mambo yaliyopitwa na wakati na hayana Manufaa yoyote kwa Mwafrika.

ii. Wakoloni walipanga kudhoofisha utamaduni wa Kiafrika na kuendeleza utamaduni wa kizungu.

c) i. Wamisheni - Ni Mawakala wa ukoloni waliotumia dini katika kufundisha kwa kuanzisha shule na taasisi mbalimbali za kidini katika kufikisha elimu ya kikoloni.


ii. Wahisani - Ni watu binafsi waliopata elimu ya kikoloni kwa kufungua shule zao zilizofuata silabasi ya kikoloni.

iii. Wamegutuka - Wameamka na kupata utambuzi juu ya jambo fulani.

iv. Wazungu weusi - Ni waafrika (Tanzania) ambao wameiga mfumo wa maisha ya kizungu.

d) Wazungu walileta mfumo mpya wa ukoloni kwa kuua mila na desturi za waafrika na kupandikiza utamaduni wao kabisa sanaa.


**Kielelezo Na.1.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 1

Katika Kielelezo Na. 1.1, mtahiniwa alionesha kuwa na uelewa wa kutosha wa kifungu cha habari hivyo alijibu vipengele vyote vinne kwa usahihi na kupata alama zote za swali hili.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 11,616 sawa na asilimia 39.80 walikuwa na ufaulu wa wastani kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 5.5. Ufaulu huu ulitokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya vipengele. Baadhi ya watahiniwa walieleza maana zisizo sahihi kwa baadhi ya maneno katika kipengele (c) (i) hadi (iv), wengine waliorodhesha mawazo yasiyo sahihi kulingana na aya ya nne ya habari waliyopewa ili kujibu kipengele (d). Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea *umuhimu wa elimu ya kikoloni*, jambo ambalo ni kinyume na mtazamo wa mwandishi ambaye alilenga kuonesha athari hasi za elimu ya kikoloni. Aidha, wapo watahiniwa walioshindwa kupendekeza kichwa sahihi cha habari katika kipengele (a) kwa kuandika kauli zisizokidhi kiini cha habari hii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika "UBAYA WA WAKOLONI" bila kuhusisha elimu yao ambayo ndiyo msingi wa habari hii, hivyo akapata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa 4,201 sawa na asilimia 14.39 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3 kwa kuwa walishindwa kutoa majibu sahihi katika vipengele vingi. Baadhi yao walionesha kukosa uelewa wa kifungu cha habari, hivyo kupendekeza kichwa cha habari kisichokuwa

sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *ELIMU YA WATANZANIA* na mwingine alinakili baadhi ya sentensi zilizopo katika kifungu cha habari katika kujibu kipengele (b), kutoa maana zisizo sahihi za maneno katika kipengele (c) ambapo mtahiniwa mmoja aliandika wamisheni ni *watu wenye kufuatilia jambo Fulani*; wahisani *ni watu wema*; wamegutuka *ni kushangazwa kwa jambo fulani;* na wazungu weusi *ni waafrika weusi*. Pia, alibainisha mawazo ya mwandishi yasiyo sahihi katika aya ya nne kwa kuandika, "*Elimu ya kikoloni ilifanikiwa kutupilia mbali mila na desturi za kishenzi zilizopitwa na wakati ili kuwakomboa waafrika*" jibu ambalo ni kinyume na uhalisia uliopo katika aya husika ya kifungu cha habari alichopewa. Kwa ujumla, watahiniwa katika kundi hili walikosa ufahamu na uelewa wa kifungu cha habari na hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi katika vipengele vingi. Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyojitosheleza katika vipengele vingi vya swali hili.



1. (a) MFUMO WA ELIMU YA KIKOLONI

(b) Wanafunzi walizuiliwa kushiriki mambo ya jadi kwa sababu
(i) Ilikuwa rahisi kuwatenganisha wanafunzi hawa na sanaa za maonyesho za jadi.

(ii) kipindi wapo likizo kulikuwa na vipo maalumu kuwangalia mienendo ya wanafunzi hao na kuhakikisha hawashiriki katika mambo ya jadi.

(c) (i) Wamisheni,
Ikiwa ina maana ya wazungu

(ii) Wahisani
Ikiwa na maana yake ni wahusika walio miliki shule hizo.





**Kielelezo Na. 1.2**: Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 1

Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha kuwa, mtahiniwa hakuelewa kifungu cha habari ipasavyo, hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi katika vipengele (b), (c) na (d) na kupata alama za chini.

#### 2.1.1.2 Swali la 2: Matumizi ya Sarufi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Sarufi* katika mada ndogo ya *Matumizi ya Mofimu*. Swali lililenga kupima uelewa wa watahiniwa katika kutambua maumbo ya mofimu katika vitenzi vya Kiswahili. Mtahiniwa alitakiwa katika kipengele (a) kufafanua tofauti kati ya nafsi na viambishi vya nafsi katika kitenzi kwa kutumia hoja sita na (b) kueleza dhima nne za viambishi katika kitenzi cha Kiswahili.

Swali lilijibiwa na watahiniwa 29,184 sawa na asilimia 100. Swali hili lilijibiwa vizuri ambapo watahiniwa 19,687 sawa na asilimia 67.46 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10 mtawalia. Chati Na. 2 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2*


Katika Chati Na. 2, watahiniwa 9,497 (32.54%) walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 3, watahiniwa 17,950 (61.51%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5 na watahiniwa 1,737 (5.95%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 6 hadi 10.

Takwimu za ufaulu wa watahiniwa zinaonesha kuwa, zaidi ya nusu ya watahiniwa (61.51%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kuwa walikuwa na uelewa usijitosheleza kuhusu mada ndogo ya *Matumizi ya Mofimu*. Watahiniwa hao waliweza kufafanua kwa usahihi baadhi ya

hoja zinazoelezea tofauti kati ya nafsi na viambishi vya nafsi katika kitenzi; na kueleza dhima nne za viambishi katika kitenzi cha Kiswahili. Baadhi ya watahiniwa walifafanua kwa usahihi hoja tatu hadi nne zinazoelezea tofauti kati ya nafsi na viambishi vya nafsi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *utofauti katika umilikishi*, *utofauti katika urejeshi*, *utofauti katika idadi*; majibu yasiyokidhi matakwa ya swali, hivyo alipata alama za wastani. Hoja sahihi zinazokidhi mahitaji ya swali hili katika kipengele (a) ni nafsi ya kwanza umoja (mimi) kiambishi (ni-), nafsi ya kwanza wingi (sisi) kiambishi (tu-), nafsi ya pili umoja (wewe) kiambishi (u-), nafsi ya pili wingi (ninyi/nyinyi) kiambishi (m-), nafsi ya tatu umoja (yeye) kiambishi (a-) na nafsi ya tatu wingi (wao) kiambishi (wa-). Katika kipengele (b), walieleza kwa usahihi dhima nne za viambishi katika kitenzi cha Kiswahili kama vile: *kuonesha nafsi*, *idadi*, *njeo*, na *urejeshi*; lakini wengi wao walishindwa kutoa mifano stahiki na kupata alama za wastani. Kwa ujumla, watahiniwa hao walikuwa na majibu yasiyojitosheleza kwa hoja au kwa ufafanuzi stahiki.

Licha ya ufaulu wa wastani wa watahiniwa katika swali hili, asilimia 32.54 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3. Ufaulu wa chini wa watahiniwa hao ulitokana na kuwa na uelewa mdogo juu ya mada ya *Matumizi ya Mofimu*. Katika kipengele (a) walishindwa kufafanua tofauti kati ya nafsi na viambishi viwakilishi vya nafsi katika kitenzi cha Kiswahili ambapo baadhi yao walieleza mambo yasiyohusiana na maumbo ya nafsi katika vitenzi: Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika, *utofauti wa kimaana*, *utofauti wa kiaina*, *utofauti wa kiwakilishwaji*, *utofauti wa kimatukio, utofauti wa urejeleo* na *utofauti wa kufikisha ujumbe*. Wengine walifafanua tofauti kati ya *mofimu* na *fonimu* au *mofolojia na fonolojia*. Katika kipengele (b) walishindwa kueleza dhima nne za viambishi katika kitenzi cha Kiswahili ambapo baadhi walitoa hoja mseto kama vile *dhima za lugha, dhima za fasihi, sifa za lugha na utata katika tungo*, hoja ambazo hazina uhusiano wowote na kiini cha swali hili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kujibu kipengele hiki aliandika; *hubadili maana ya kitenzi, hubadili kategoria ya neno au kitenzi*, *hudokeza nia au lengo la tendo* na *hutaja kifaa*. Mtahiniwa mwingine aliandika, *kurithisha amali za jamii, kuelimisha jamii* na *kuburudisha jamii* badala ya kueleza dhima nne za

viambishi katika kitenzi cha Kiswahili kama vile; kuonesha nafsi mbalimbali kwa mfano; tumeibiwa- **tu**-nafsi ya kwanza wingi, alimuona- **a-** nafsi ya tatu umoja, kuonesha njeo/wakati mfano, utanipa- **ta**- wakati ujao, alikuja **-li**- wakati uliopita, kuonesha hali mbalimbali mfano, hali ya masharti, akija ataniona- **ki**- masharti, kuonesha urejeshi mfano, kilichonunuliwa **cho**- urejeshi, kuonesha ukanushi mfano, haondoki **ha**- ukanushi, kuonesha kauli mbalimbali mfano, limisha **ish**- kauli ya kutendesha na kuonesha kiambishi tamati maana mfano, anachez**a** **a**- kiambishi tamati maana. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.



a (i) Nafci huweza kuwa kama nomino kati ka sentenci hasa katika Utumizi wa maji na.

(ii) Viambichi hupachikwa mwanzo mwa mzi zi wa neno na baada ya Mzizi wa neno lakini Viambichi Viwakilichi nafci husimama baada ya nomino katika sentenci.

(iii) Viambichi Viwakilichi vya nafci hutumi ka kama njeo katika sentenci lakini nafci haiwezi kutumika.

(iv) Nafci huonyesha jinci tendo lilivyotend eka kwa kuangalia kanuni za kutenda, kutendeka, kutendeana lakini Viambichi Vi wakilichi nafci katika kitenzi haionyeshi.

(v) Viambichi Viwakilichi vya nafci huweza kuonyesha Mzizi wa neno katika kitenzi lakini nafci haiwezi kuonyesha.

(vi) Nafci haiwezi kudondoshwa kwa M neno katika sentenci lakini viambichi Viwakilichi vya nafci katika kitenzi hu weza kudondosha baadhi ya maneno.

**Kielelezo Na. 2.1**: Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 2

Katika Kielelezo Na. 2.1, mtahiniwa alielezea isivyo tofauti kati ya nafsi na viambishi viwakilishi vya nafsi katika kitenzi cha Kiswahili katika kipengele (a) kwa kuelezea matumizi ya viambishi nafsi kama vile *kusimama kama nomino, kutumika kama njeo, kuonesha tendo lilivyotendeka, kuonesha mzizi*, na *kudondosha maneno*; majibu yasiyokidhi matakwa ya swali, hivyo kupata alama 0.

Hata hivyo, watahiniwa wachache (5.95%) walifaulu vizuri kwa kuwa walijibu kwa usahihi vipengele vingi vya swali hili na kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10. Ufaulu mzuri wa watahiniwa hao ulitokana na kuwa na maarifa kuhusu matumizi ya mofimu katika lugha ya Kiswahili. Watahiniwa hao waliweza kufafanua kwa usahihi tofauti kati ya nafsi na viambishi viwakilishi vya nafsi katika kitenzi cha Kiswahili katika kipengele (a) kama vile:

> *nafsi ya kwanza umoja (mimi) na kiambishi (ni-), nafsi ya kwanza wingi (sisi) na kiambishi (tu-), nafsi ya pili umoja (wewe) na kiambishi (u-), nafsi ya pili wingi (ninyi/nyinyi) na kiambishi (m-), nafsi ya tatu umoja (yeye) na kiambishi (a-) na nafsi ya tatu wingi (wao) na kiambishi (wa-).*

Aidha, katika kipengele (b) walieleza kwa usahihi dhima nne za viambishi katika kitenzi cha Kiswahili kama vile:

> *kuonesha nafsi mbalimbali kwa mfano; <u>tu</u>meibiwa- (tu-) nafsi ya kwanza wingi, <u>a</u>limuona (a-) nafsi ya tatu umoja, huonesha njeo/wakati mfano, u<u>ta</u>nipa (-ta-) wakati ujao, a<u>li</u>kuja (-li-) wakati uliopita, huonesha hali mbalimbali mfano, hali ya masharti, a<u>ki</u>ja ataniona (-ki-) masharti, huonesha urejeshi mfano, kili<u>cho</u>nunuliwa (-cho-) urejeshi, huonesha ukanushi mfano, <u>ha</u>ondoki (ha-) ukanushi, huonesha kauli mbalimbali mfano, lim<u>ish</u>a (-ish-) kauli ya kutendesha na huonesha kiambishi tamati maana mfano, anachez<u>a</u> (-a) kiambishi tamati maana.*

Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kutokana na kutoa majibu sahihi yaliyokidhi matakwa ya swali hili.

02. a) Utofauti kati ya nafsi na viambishi viwakilishi vya nafsi katika kitenzi kama ifuatayo:-

i) Nafsi ya kwanza umoja ambayo "mimi"
Mfano- Nafsi ya kwanza umoja
(I) Mimi
- Kiambishi kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja (II) Ninalima (Ni)


ii) Nafsi ya pili umoja ambayo mzingi wake ni neno "wewe"
Mfano- Nafsi ya pili umoja
(I) wewe
- kiambishi kiwakilishi cha nafsi ya pili umoja (II) Unasoma. - (U)

iii) Nafsi ya tatu umoja ambayo mzingi wake ni neno "yeye"
Mfano - Nafsi ya tatu umoja

(I) yeye

- kiambishi kiwakilishi cha nafsi ya tatu umoja ni Anasoma - (A)

IV) Nafsi ya kwanza wingi ambayo mzingi wake ni neno "sisi"
Mfano- Nafsi ya kwanza wingi
(I) sisi
- kiambishi kiwakilishi cha nafsi hii ni (II) Tunasoma - (Tu)



Q2. a) i) Nafsi ya pili wingi ambayo mzizi wake ni neno "ninyi"
Mfano:
- Nafsi ya pili wingi
(i) ninyi
- Kiambishi kiwakilishi cha nafsi ya pili wingi ni
(ii) Mnasoma - (m)

ii) Nafsi ya tatu wingi ambayo mzizi wake ni neno "wao"
Mfano:- Nafsi ya tatu wingi
(i) Wao
- Kiambishi kiwakilishi cha nafsi hii ni
(ii) wanasoma (wa)

b) i) Kudokeza wakati
Kwa mfano a) Anacheza - wakati uliopo
b) Atacheza - wakati ujao
c) Alicheza - wakati uliopita.

ii) Kudokeza nafsi
Kwa mfano i) Nafsi ya kwanza - Ninaimba
ii) Nafsi ya pili - Unaimba
iii) Nafsi ya tatu - Anaimba

iii) Kudokeza hali ya masharti
Kwa mfano - Ikicheza
- Ikiimba
iv) Kudokeza kauli mbalimbali za kutenda
Kwa mfano. i) Kauli ya kutenda - Analima.
ii) Kauli ya kutendwa - Analimwa.


**Kielelezo Na. 2.2**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 2

Katika Kielelezo Na. 2.2, mtahiniwa alieleza kwa usahihi tofauti kati ya nafsi na viambishi viwakilishi vya nafsi katika kitenzi kwa kipengele (a) na kueleza kwa usahihi dhima nne za viambishi katika kitenzi cha Kiswahili katika kipengele (b) na kupata alama zote katika swali hili.

### 2.1.1.3 Swali la 3: Matumizi ya Sarufi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Sarufi* mada ndogo ya *Kauli za Kiswahili* na lililenga kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu kauli mbalimbali zinazodhihirika katika vitenzi vya Kiswahili. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika vitenzi alivyopewa katika kauli zilizowekwa kwenye mabano kisha kubainisha viambishi vyake.


Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote (29,184) waliofanya mtihani huu. Uchambuzi unaonesha kuwa, swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwani watahiniwa 25,787 sawa na asilimia 88.36 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Chati Na. 3 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




. **Chati Na. 3:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3*

Katika Chati Na. 3, watahiniwa 3,397 (11.64%) walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 3, watahiniwa 6,523 (22.35%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5 na watahiniwa 19,264 (66.01%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 6 hadi 10.

Watahiniwa wengi (66.01%) waliweza kuandika kwa usahihi vitenzi walivyopewa katika kauli (3 – 5) zilizowekwa kwenye mabano kisha walibainisha viambishi vya kauli hizo kwa usahihi na kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Kati yao, asilimia 28.19 walipata alama za juu kuanzia 8 hadi 10 kutokana na kumudu kuandika kwa usahihi vitenzi (4 – 5) walivyopewa katika kauli zilizowekwa kwenye mabano kisha kubainisha kwa usahihi viambishi vya kauli hizo. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika kwa usahihi vitenzi katika kauli alizopewa kisha kubainisha kwa usahihi viambishi vya kauli hizo kama (a) *pangisha* kiambishi cha kauli (-*ish*-), (b) *pigiana* kiambishi cha kauli (-*ian*-), (c) *saidiana* kiambishi cha kauli (-*an*-) na (d) *chomewa* kiambishi cha kauli (-*ew*-). Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.


3. a) Panga Kauli ya Kutendesha ni Pangisha
Pang-ish-a, kiambishi cha Kauli ni -ish-

b) Piga Kauli ya Kutendeana Inakuwa Pigiana
Pig-ian-a
Kiambishi Cha Kauli ni -ian-

c) Saidia Kauli ya Kutendana inakuwa Saidiana
Saidi-an-a
Kiambishi cha kauli ni -an-


d) Choma Kauli ya Kutendewa inakuwa Chomewa
Chom-ew-a
Kiambishi cha Kauli ni -ew-

**Kielelezo Na. 3.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 3

Katika Kielelezo Na. 3.1, mtahiniwa aliandika kwa usahihi kauli za vitenzi (i) hadi (iv) pamoja na kubainisha kwa usahihi viambishi vya kauli hizo na kupata alama zote.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 6,523 sawa na asilimia 22.35 walipata alama kuanzia 3.5 hadi 5.5. Ufaulu wa wastani wa watahiniwa ulitokana na kushindwa kuandika baadhi ya kauli za vitenzi walivyopewa na wengine walibainisha kauli hizo kwa makosa. Wapo walioandika baadhi ya vitenzi walivyopewa katika kauli zilizowekwa kwenye mabano kwa usahihi na kubainisha viambishi vya kauli husika katika baadhi ya vipengele huku wakishindwa kufanya hivyo katika vipengele vingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kwa usahihi kauli za vitenzi (a) *panga* kuwa ni *pangisha* na kiambishi cha kauli hiyo ni **-ish-**; (b) *piga* kauli yake ni *pigiana* na kiambishi cha kauli hiyo ni **-an**-; na (d) *choma* kauli yake ni *chomewa* na kiambishi cha kauli hiyo ni **w**; majibu ambayo si sahihi kulingana na kauli alizopewa, hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (11.64%) waliokuwa na ufaulu hafifu walishindwa kuandika kauli za vitenzi walivyopewa na kubainisha kauli za vitenzi hivyo kwa makosa. Baadhi yao waliandika vitenzi vingine tofauti na walivyopewa na kubainisha kauli kulingana na vitenzi hivyo kinyume na matakwa ya swali hili. Wengine waliandika kauli za vitenzi walivyopewa kwa makosa na kubainisha viambishi vya kauli kimakosa na hivyo kupata alama za chini. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kauli za vitenzi alivyopewa kama ifuatavyo: (a) *kupangishiwa* kiambishi cha kauli "*sha*", (b) *kupigana* kiambishi cha kauli ni "*na*", (c) *kusaidiwa* kiambishi cha kauli "*sa*" na (d) *kuchomewa* kiambishi cha kauli "*ku*" ambazo si kauli sahihi kulingana na matakwa ya swali hili. Mtahiniwa huyo alitakiwa kuandika kauli za vitenzi na kubainisha viambishi vya kauli hizo kama ifuatavyo: (a) Pangisha - pang-<u>ish</u>-a - (-ish-) - kiambishi tamati - kauli ya kutendesha, (b) Pigiana - pig- <u>ian</u>-a (-ian-) - kiambishi tamati - kauli ya kutendeana (c) Saidiana saidi-<u>an</u>-a (-an-) - kiambishi tamati - kauli ya kutendeana na (d) Chomewa - chom-ew-a (-ew-) - kiambishi tamati - kauli ya kutendewa. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.


3 Andika vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizowekwa
kwenye mabano kisha kuainisha viambishi vya kauli
a) Panga (kutendesha)
Baba anakata mti kwa kutumia Panga.
b) Piga (kutendeana)
watoto wanapigana kwa kutumia fimbo.
3 c) Saidia (kutendeana)
mtoto anamsaidia baba kuchunga ng'ombe
d) Choma (kutendwa)
mpishi anachoma nyama ya mbuzi.


**Kielelezo Na. 3.2**: Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 3

Katika kielelezo Na. 3.2, mtahiniwa alitunga sentensi kwa kutumia vitenzi alivyopewa badala ya kuandika vitenzi hivyo katika kauli zilizowekwa kwenye mabano kisha kubainisha viambishi vya kauli husika.

### 2.1.1.4 Swali la 4: Utumizi wa Lugha

Swali hili lilitoka katika mada ya *Utumizi wa Lugha* katika mada ndogo ya *Lugha ya Mazungumzo* na *Lugha ya Maandishi*. Swali lililenga kupima uchambuzi na lilimtaka mtahiniwa kufafanua mambo matano yanayodhihirisha tofauti kati ya lugha ya kuzungumza na lugha ya kuandika katika kufikisha ujumbe kwa hadhira.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote (29,184) waliofanya mtihani huu. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri zaidi ambapo, watahiniwa 28,577 sawa na asilimia 97.92 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 4*

Katika Chati Na. 4, watahiniwa 607 (2.08%) walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 3, watahiniwa 8,732 (29.92%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5 na watahiniwa 19,945 (68.00%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6 hadi 10.

Watahiniwa wengi (68.00%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa hao walionesha kuwa na umahiri wa kutosha juu ya mada ya *Matumizi ya Lugha*, kwa kuwa waliweza kutumia mifano sahihi katika kufafanua mambo matano yanayodhihirisha tofauti kati ya lugha ya mazungumzo na lugha ya kuandika katika kufikisha ujumbe kwa hadhira. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili waliojibu vizuri swali hili walionesha tofauti kati ya lugha ya mazungumzo na lugha ya kuandika kwa hoja kama: *lugha ya mazungumzo hutumia gharama nafuu/hakuna gharama kabisa* lakini *lugha ya kuandika huwa na gharama kubwa*, *lugha ya mazungumzo huweza kufanyiwa marekebisho ya papo kwa papo* lakini *lugha ya maandishi haiwezi kufanyiwa marekebisho ikishaandikwa*, *lugha ya mazungumzo hutumia maneno yasiyo rasmi* lakini *lugha ya maandishi hutumia lugha rasmi*, *lugha ya mazungumzo haihitaji maandalizi ya muda mrefu* lakini *lugha ya maandishi huhitaji maandalizi ya muda mrefu* na hoja nyinginezo ambazo ni sahihi. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu katika swali hili.

4. Lugha ya Kuzungumza; Ni lugha ambayo uwasilishwaji wake hutumia mazungumzo baina ya mzungumzaji (fanani) na Msikilizaji au wasikilizaji (Hadhira). na
Lugha ya Kuandika; Ni lugha ambayo huwasilishwa Kwa Maandishi. Zifuatazo ni tofauti Kati ya lugha ya Kuzungumza na lugha ya Kuandika.

Uwasilishwaji; Lugha ya Kuzungumza huwasilishwa Kwa njia ya mazungumzo ambapo mzungumzaji (fanani) huzungumza na Msikilizaji au Hadhira husikiliza lakini Lugha ya Kuandika Huwasilishwa Kwa maandishi ambapo mwandishi huandika na msomaji au wasomaji husoma Kazi hiyo.

Chanzo na ukomo; Lugha ya Kuzungumza Chanzo chake ni mzungumzaji yaani fanani na ukomo wake ni msikilizaji yaani Hadhira ambaye ndiye humsikiliza Mzungumzaji lakini lugha ya Kuandika Chanzo chake ni Mwandishi ambaye huandika na ukomo wake ni Msomaji asomaye Kazi ya mwandishi.

Umri; lugha ya Kuzungumza ni Kongwe Kwani imekuwepo Kabla ya ugunduzi wa maandishi Lakini lugha ya Kuandikwa sio Kongwe Kama lugha ya Kuzungumza Kwani Imeanza Kutumika baada ya ugunduzi wa Maandishi.

Upokeaji wa mabadiliko; lugha ya kuzungumza hupokea mabadiliko ya papo kwa papo kwa sababu huwa na hadhira hai hivyo kuweza kubadilika kutokana na mkutadha lakini lugha ya kuandika haipokei mabadiliko ya papo kwa hapo kwani ikishaandikwa si rahisi kurekebishwa hata kama kuna makosa au mapungufu.

Maandalizi; lugha ya kuzungumza haihitaji maandalizi kwani fanani huweza kuongea mahali popote ili mradi kuna hadhira tofauti na lugha ya kuandika ambayo huhitaji maandalizi kama vile kuwa na vifaa vya kuandikia kama vile kalamu, karatasi au daftari n.k.

Hata hivyo; aina hizi za lugha kila moja huwa na changamoto yake kwani lugha ya mazungumzo haina kumbukumbu kwani hakuna nyaraka yoyote inayopatikana baada ya mazungumzo, vivyo hivyo lugha ya kuandika hubagua kwani huwahusisha wanaojua kusoma na kuandika tu; hivyo kuwa mali ya watu wachache ndani ya jamii.


**Kielelezo Na.4.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 4


Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu mazuri ya mtahiniwa aliyetofautisha kwa usahihi lugha ya mazungumzo na lugha ya kuandika katika kufikisha ujumbe kwa kuzingatia *uwasilishaji, chanzo na ukomo, umri, upokeaji wa mabadiliko*, na *maandalizi*. Kwa ujumla, mtahiniwa huyo alionesha umahiri wa hali ya juu kwa kufafanua vizuri mambo matano yanayodhihirisha tofauti hizo na kutoa mifano dhahiri.

Aidha, asilimia 29.92 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 5.5. Watahiniwa hao walitoa majibu yasiyojitosheleza katika kutofautisha lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi ambapo walitoa majibu yenye mapungufu madogo madogo hususan kutoa mifano isiyo sahihi

kwa baadhi ya hoja, kutoa ufafanuzi usiojitosheleza kwa baadhi ya hoja, hivyo walipata alama za wastani. Hii ilitokana na kukosa umahiri wa kutosha katika dhana nzima ya uwasilishaji wa fikra/dhana kwa njia ya maandishi au mazungumzo.

Hata hivyo, watahiniwa wachache (607) sawa na asilimia 2.08 walipata alama hafifu kuanzia 0 mpaka 3 kutokana na kukosa maarifa ya kutosha juu ya lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi. Baadhi yao waliweza kufafanua tofauti chache na kutoa mifano isiyokidhi matakwa ya swali. Wengine walishindwa kabisa kufafanua tofauti hata moja na kushindwa kutoa mifano yenye kudhihirisha tofauti kati ya lugha ya mazungumzo na lugha ya kuandika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua jambo moja tu (upokeaji wa mabadiliko) ambalo huzingatiwa katika kufikisha ujumbe kwa hadhira kati ya njia ya mazungumzo au maandishi. Aidha, hoja zingine alizotoa mtahiniwa huyo zilihusu mambo muhimu ya kuzingatia katika mazungumzo kama: *mada ya mazungumzo*, *uhusiano baina ya wazungumzaji*, *muktadha*, *lengo la mazungumzo* na *njia ya mawasiliano*; majibu ambayo ni kinyume kabisa na matakwa ya swali hili, hivyo kupata alama za chini. Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.


04. Lugha :- Ni mfumo wa sauti za nasibu
zilizo beba maana na zilizo kubalika katika
jamii ya watu fulani katika mawasiliano
kuna aina mbili za uwasilishaji wa lugha
hii i/ Lugha ya kuandikwa - Hii ni aina ya
lugha ambayo huwasilishwa kwa njia ya kuandikwa
na lugha ya kuzungumza - Hii ni aina
ya lugha inayowasilishwa kwa kutumia njia
ya kuongea / Njia ya mdomo. Kwa kutumia
hoja tano zifuatazo ni njia mambo yanayo
dhihirisha utofauti kati ya lugha ya
mazungumzo na lugha ya mawasiliano -
kuandika kama ifuatavyo


Kimuundo:- Miongoni mwa mambo yanayojitokeza tofauti wepo baina ya Lugha ya mazungumzo na Lugha ya Maandishi ni pamoja na Uwasilishwaji wa Lugha ya mazungumzo hii Uwasilishwaji wake Unakuwa kwa mdomo wakati Maandishi inakuwa kwa njia ya Maandishi / Lugha ya Mazungumzo huwa inaweza kuwa ana moja kwa moja wakati Lugha ya Maandishi ikabakia kuwa ya kimedia media.

Mtindo:- Katika nadharia hii inatoa tofauti kubwa katika ya Lugha ya Mazungumzo na lugha ya kuandikwa kwani mtindo unaotumika katika lugha ya mazungumzo ni mtindo wa mdomo wakati lugha ya kuandikwa hutumia Lugha Maandishi katika Uwasilishwaji wake.

Kimaudhui:- Nadharia hizi mbili zinatofautiana katika mtindo wa kimaudhui kwani Lugha ya Matamshi huwa na wahusika Wachache wakati Lugha ya Maandishi huwa na wahusika anaotumia wahusika wengi kwenye kufikisha ujumbe wake.

Kiuwasilishwaji:- Ninamna jinsi Uwasilishwaji wa kazi hizi mbili jinsi zinavyo tofautiana katika Uwasilishaji wake Unakuwa tofauti kwani moja utumia Maandishi na Nyingine hutumia Mazungumzo.

Kimaana:- Hii hutofautiana na hata pia kwenye Maana hapo zote huwa zinatoa Lugha Ufani kulingana na jambo la wetu hivyo jinsi kitu nauyotamka tofauti na

**Kielelezo Na. 4.2**: Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 4.

Katika Kielelezo Na. 4.2, mtahiniwa alitofautisha lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi kwa kuzingatia *muundo, mtindo, maudhui*, na *uwasilishaji* kinyume na mahitaji ya swali hili na kupata alama za chini. Mtahiniwa alitakiwa kufafanua mambo yanayodhirisha tofauti hizo katika uwasilishaji pekee kama vile ujuzi wa

kusoma/kuandika, gharama, marekebisho/mabadiliko, matumizi ya lugha rasmi na maandalizi katika uwasilishaji wake.


### 2.1.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAREFU

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali manne ya insha. Swali la sita (6) lilikuwa ni la lazima. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu na kila swali lilikuwa na alama 20.

#### 2.1.2.1 Swali la 5: Uandishi wa Insha

Swali hili lilitoka katika mada ya *Utungaji*, mada ndogo ya *Uandishi wa Insha* na lililenga kupima uundaji. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika insha isiyozidi ya maneno 400 na isiyopungua maneno 350 kuhusu ujangili nchini Tanzania.

Uchambuzi wa takwimu za ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa, swali hili lilijibiwa na watahiniwa 20,312 (69.60%) kati ya watahiniwa 29,184 waliofanya mtihani. Swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri ambapo watahiniwa 18,265 sawa na asilimia 89.92 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama 7 hadi 20. Chati Na. 5 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5*

Katika Chati Na. 4, watahiniwa 2,047 (10.08%) walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5, watahiniwa 4,758 (23.42%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5 na watahiniwa 13,507 (66.50%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 12 hadi 20.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, zaidi ya nusu ya watahiniwa (13,507) sawa na asilimia 66.50 walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu uandishi wa insha, hivyo walipata alama kuanzia 12 hadi 20 katika swali hili. Kati yao, watahiniwa 2,090 sawa na asilimia 10.29 walijibu vizuri zaidi na kupata alama za juu kuanzia 18 hadi 20. Kwa ujumla, watahiniwa hao waliweza kuandika insha iliyozingatia vyema vigezo vyote muhimu kama vile; kuandika kichwa cha insha kwa herufi kubwa, utangulizi mzuri unaofafanua maana ya ujangili, na katika kiini walifafanua vizuri athari za ujangili, sababu za ujangili na kutoa maoni na ushauri kuhusu uthibiti wa ujangili na walitoa hitimisho zuri linaloendana na kichwa cha insha "Ujangili nchini Tanzania." Aidha, watahiniwa hao waliandika insha kwa kuzingatia alama sahihi za uandishi na matumizi ya lugha sanifu. Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa katika swali hili.

5. UJANGILI NCHINI TANZANIA.

Ujangili ni hali ya mtu au Kikundi Cha Watu Kuvamia hifadhi za wanyama mbalimbali na Kufanya uhalifu Kwa Kuwasafirisha Kinyemera wanyama hao. Tanzania ni muongoni mwa mataifa Ulimwenguni ambayo yana vivutio vingi vya utalii. Mfano, hifadhi za wanyama, mito, bahari, milima na mabonde. Katika upande wa hifadhi za wanyama, zimesheheni aina mbalimbali za wanyama mfano, simba, tembo, nyati (mbogo). Kutokana na uwepo wa wanyama hao imesababisha wimbi la Ujangili kuwalo. Sababishwa na sababu zifuatazo:-

Uingiaji holela wa wageni kutoka mataifa mbalimbali ulimwenguni. Tanzania kwa kuwa ni Kisiwa cha amani, huweza kupokea wageni mbalimbali kutoka mataifa mbalimbali. Mfano, Ujerumani, Uingereza na Marekani ambao baadhi yao si watu wema na ndio chanzo cha ujangili. Hivyo Serikali izingatie wageni waingiao nchini.

Kukosekana kwa ulinzi madhubuti katika hifadhi za wanyama. Mfano. Bungi-Chato, Serengeti, Ngorongoro, Ulinzi uliopo katika hifadhi hizo siyo madhubuti ukilinganisha na mataifa mengine ulimwenguni na hivyo kusababisha Kukithiri kwa ujangili ~~ulimwengu~~ nchini Tanzania.

Hivyo kutokana na ongezeko la ujangili nchini imesababisha athari hasi zifuatazo:-

Kushuka kwa pato la taifa katika sekta ya Utalii; hii imesababishwa na kutoweka kwa baadhi ya wanyama ambao ni nyenzo muhimu katika sekta ya utalii ndani ya Taifa. Mfano, tembo, swala, nyati, badala ya kuwauza tukapata kipato badala yake

5\. wanachukuliwa Kinyemera hivyo kushusha pato la taifa.

Kutoweka na kupoteza wanyama na maliasili muhimu katika wizara ya utalii. Hii hii ni athari ya ujangili ambayo imesababisha Tanzania kupoteza baadhi ya wanyama muhimu, mfano Mbogo, tembo twiga, hawa ni miongoni mwa wanyama ambao wanaleta kuwa hasara kwa Taifa, linapowapoteza.

Kupungua na Kushuka Kwa idadi ya watalii wa ndani na hata nje ya Taifa. Ujangili umeweza Kusababisha Kupungua na Kushuka Kwa idadi ya watalii waingiao nchini. Siyo wale tu wa ndani ya Taifa bali hata wale wa kutoka nje ya Taifa. Hii ni Kutokana na kutoweka na kupungua kwa idadi ya wanyama nchini Tanzania.

Zifuatazo ni hatua madhubuti zinazopaswa kuchukuliwa ili Kuondoa suala la ujangili nchini Tanzania.

Kuongeza ulinzi imara katika hifadhi zote za Taifa. Ili kuhakikisha tunaondokana na suala hili ni vema serikali Kuhakikisha inaongeza ulinzi katika hifadhi zote za Taifa. Mfano, kuanzisha kambi za Kijeshi katika hifadhi hizo ili ziwasaidie katika ulinzi. Kwa Kufanya hivyo itasaidia kupunguza na kuondoa tatizo la ujangili nchini Tanzania.

Kuanzisha na kurasmisha Sheria madhubuti juu ya ujangili na kuzisimamia vema. Ili kuondokana na tatizo la ujangili nchini ni vema serikali kuanzisha Sheria kali ambazo zitasaidia katika kupunguza suala hili la ujangili. Mfano. Kwa yeyote atakayebainika anajihusisha na suala hilo adhabu yake ni kifungo miaka thelathini (30) itakayoambatana na adhabu ya faini kwa mujibu wa katiba.

Hivyo basi; Ujangili unapaswa kudhibitiwa vikali ili kuleta uchumi bora ndani na hata nje ya nchi kupitia sekta ya utalii.


**Kielelezo Na. 5.1:** Sampuli ya Jibu Sahihi katika Swali la 5

Katika Kielelezo Na. 5.1, mtahiniwa aliweza kuandika insha kuhusu “Ujangili Nchini Tanzania” kwa kueleza athari hasi na namna ya

kuukabili ujangili nchini kwa usahihi na kupata alama za juu, jambo linaloonesha kuwa alikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu uandishi wa insha. Hata hivyo, mtahiniwa alikosea kwa kuandika neno *TANZAMA* badala ya TANZANIA.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 4,758 (23.42%) walikuwa na ufaulu wa wastani ambapo walipata alama kuanzia 7 hadi 11.5. Majibu ya watahiniwa katika kundi hili yanaonesha kutokujitosheleza kwa baadhi ya mambo muhimu ya kuzingatiwa katika uandishi wa insha. Watahiniwa hao waliandika insha kwa kuzingatia kichwa cha insha yaani "Ujangili Nchini Tanzania" lakini walishindwa kuzingatia baadhi ya vipengele muhimu katika uandishi wao. Baadhi yao waliandika bila kuzingatia idadi sahihi ya maneno, ufafanuzi wa kichwa cha habari (utangulizi), sababu za ujangili, madhara na namna ya kuukabili ujangili nchini Tanzania na hivyo walipata alama za wastani. Wengine waliandika insha bila kuzingatia mpangilio ulio na mantiki na muundo wa aya, hivyo kukidhi sehemu ndogo ya matakwa ya swali na kupata alama za wastani katika swali hili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika insha isiyo na ufafanuzi wa kichwa cha insha, kwenye kiini alitoa baadhi ya hoja zisizo na uhalisia kwa kueleza madhara ya ujangili kwa majangili badala ya madhara yao kwa taifa, na kwenye hitimisho alieleza mauaji ya albino kuwa ni matokeo ya ujangili kinyume na matakwa ya kichwa cha insha.

Hata hivyo, watahiniwa wachache (2,047) sawa na asilimia 10.08 waliojibu swali hili walipata ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5. Ufaulu hafifu ulitokana na watahiniwa hao kuandika insha bila kuzingatia uandishi wa kichwa cha insha kwa herufi kubwa, utangulizi usioendana na kichwa cha insha na kwenye kiini cha insha walitoa hoja zisizoendana na ujangili nchini Tanzania. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika insha kuhusu maswala ya kimtambuka kama *ajali za barabarani*, *wizi wa majumbani*, *ubakaji, ulawiti*, na wengine waliandika *barua au matangazo mbalimbali* kinyume na matakwa ya swali badala ya kuandika insha kuhusu "Ujangili nchini Tanzania" na hivyo walipata alama za chini. Kielelezo Na. 5.2 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili na kupata alama 0.




**Kielelezo Na. 5.2:** Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 5

Katika Kielelezo Na. 5.2, mtahiniwa aliandika insha isiyokidhi vigezo stahiki vya insha kama kichwa cha insha, utangulizi usio sahihi kuhusu maana ya ujangili, katika kiini alielezea uovu mbalimbali na madhara yake katika jamii kama *ubakaji, ukatili, wizi wa mali za watu/umma, uuaji* na *kunyonga;* mambo yasiyohusiana na ujangili nchini Tanzania na katika hitimisho alitoa hoja zisizoendana na insha aliyoandika.

#### 2.1.2.2 Swali la 6: Tafsiri na Ukalimani

Swali hili lilitoka katika mada ya *Tafsiri na Ukalimani*, mada ndogo ya *Tafsiri*. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote 29,184 waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa la lazima. Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa katika kutafsiri matini kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza mbinu nne anazoweza kutumia katika kutafsiri matini iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza.

Uchambuzi wa takwimu za ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa, swali hili ndilo lililokuwa na ufaulu wa chini ikilinganishwa na maswali yote yaliyotahiniwa katika mtihani huu ambapo watahiniwa 17,736 sawa na asilimia 60.77 ndio walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 7 hadi 20. Jedwali Na. 2 linaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

**Jedwali Na. 2: Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa**

| Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0 – 6.5 | 11,448 | 39.23 |
| 7 - 11.5 | 2,590 | 8.87 |
| 12 -20 | 15,146 | 51.90 |

Katika Jedwali Na. 2, watahiniwa 11,448 (39.23%) walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5, watahiniwa 2,590 (8.87%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5 na watahiniwa 15,146 (51.90%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 12 hadi 20.

Uchambuzi unaonesha kuwa nusu ya watahiniwa (51.90%) walijibu vizuri swali hili na hivyo walipata alama kuanzia 12 hadi 20. Miongoni mwao, watahiniwa 2,260 sawa na asilimia 7.74 walipata alama za juu kuanzia 18 hadi 20 kutokana na kueleza kwa usahihi mbinu nne zinazotumika kutafsiri matini iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza. Watahiniwa hao waliweza kueleza kwa usahihi mbinu anazoweza kutumia mfasiri katika kutafsiri matini iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza kwa hoja kama: *tafsiri ya neno kwa neno* yaani maneno kufasiriwa yakiwa

pweke pweke yakizingatia maana ya msingi ya lugha chanzi; *tafsiri sisisi* inayozingatia sarufi hasa sintaksia ya lugha lengwa; *tafsiri ya kisemantiki* inayoegemea maana na muundo wa matini chanzi; na *tafsiri ya kimawasiliano* inayozingatia kueleweka kwa ujumbe kwa hadhira lengwa. Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kwa kukidhi matakwa ya swali na hivyo alipata alama za juu.

6 Tafsiri ni kitendo cha kuhawilisha ujumbe ulio katika lugha ya maandishi kutoka lugha moja yaani Lugha Chanzi (LC) kwenda lugha Lengwa (LL). Mara nyingi kazi ya tafsiri hufanywa na mfasiri aliye na taaluma hii ya tafsiri kwani hupaswa azingatie hatua mbalimbali wakati wa kufasiri mfano asome matini chanzi, atambue lengo na mada ya matini chanzi pia ajue mbinu atakayotumia katika kutafsiri matini yake. Vilevile kazi ya tafsiri hujumuisha lugha mbili tofauti mfano Kingereza na Kiswahili. Hivyo kutafsiri matini aliyopewa Juma kutoka Kiswahili kwenda Kingereza huweza kutumia mbinu zifuatazo.

Tafsiri ya neno kwa neno, hii ni mbinu ya tafsiri ambayo maneno yaliyo katika lugha chanzi huhawilishwa kiupwekeupweke bila kujali maana katika lugha lengwa. Katika mbinu hii vipengele vya lugha kama vile majimu hupelekwa kwenye lugha lengwa kama vilivyo. Mfano

› Don't cry over the split milk - Kiingereza
Usilie juu ya kumwagika maziwa - Kiswahili.
Dead line - Kiingereza
Kifo mstari - Kiswahili.

Hivyo tafsiri hii huwa tafsiri potofu kwani lugha lengwa hushindwa kueleweka ujumbe uliokusudiwa na mwandishi wa lugha chanzi.

Tafsiri sisisi, hii ni mbinu ya tafsiri ambayo maneno katika matini chanzi hufasiriwa kiupwekeupweke kwa kuzingatia maana na sarufi ya lugha lengwa bila kujali muktadha

6 wa lugha chanzi. Mfano
Mawenzi teacher presents his school - Kiingereza
Mawenzi mwalimu wakilisha yake shule - Kiswahili
Hivyo mbinu hii ya tafsiri hupelekea tafsiri potofu kwani msomaji wa matini lengwa hupaswa kuwa makini sana ili aweze kuelewa matini na ujumbe husika.
Tafsiri ya kisemantiki hii ni mbinu ya tafsiri inayoegemea zaidi kwa mwandishi ambayo vipengele vidogovidogo kama vile maana hutiliwa maanani. Mbinu hii hutumika zaidi katika matini za kisiasa, kisayansi na zaidi katika matini elezi kwani mwandishi hueleza zaidi hisia zake. Mfano.
I feel cold - Kiingereza
Najisikia baridi - Kiswahili
Lend me your ears - Kiingereza
Niazime masikio yako - Kiswahili
Hivyo mbali na matumizi makubwa ya mbinu hii ya tafsiri vilevile mbinu hii hutoa tafsiri potofu kwani mara nyingine hadhira lengwa hushindwa kuelewa kwa urahisi ujumbe uliokusudiwa na mwandishi.
Tafsiri ya kimawasiliano, hii ni mbinu ya tafsiri ambayo huegemea kwa hadhira lengwa ili kueleweka kwa ujumbe. Hii nd-iyo mbinu inayotumiwa na wataalamu wengi wakati wa shughuli za tafsiri na pia ndiyo nyenzo kuu katika kutafsiri matini mbalimbali. Mfano.
Don't cry over split milk - Kiingereza
Maji yakimwagika hayazoleki - Kiswahili

**Kielelezo Na. 6.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 6

Katika Kielelezo Na. 6.1, mtahiniwa alieleza mbinu nne za tafsiri anazoweza kuzitumia katika kutafsiri matini iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza kwa usahihi. Hata hivyo,

mfano wa mbinu ya *tafsiri sisisi* haukuwa sahihi kwani alitumia mbinu ya tafsiri ya neno kwa neno bila kuzingatia sarufi ya lugha lengwa.


Kadhalika, watahiniwa 2,590 sawa na asilimia 8.87 walikuwa na ufaulu wa wastani kwa kuwa walitoa majibu yasiyojitosheleza na hivyo kupata alama kuanzia 7 hadi 11.5. Watahiniwa hao waliweza kueleza kwa usahihi baadhi ya mbinu za tafsiri na kushindwa kueleza mbinu nyingine kama ilivyotakiwa. Vilevile, watahiniwa wengine katika kundi hili waliweza kutaja kwa usahihi mbinu zote za tafsiri lakini maelezo na mifano yao haikujitosheleza kukidhi matakwa ya swali, hivyo walipata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kwa usahihi mbinu ya kisemantiki na kimawasiliano lakini katika kuelezea mbinu ya tafsiri sisisi, maelezo yake hayakuwa sahihi kwani yaliegemea mbinu ya neno kwa neno na kupata alama pungufu katika swali hili.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 11,448 sawa na asilimia 39.23 walitoa majibu yasiyojitosheleza, na hivyo walipata alama hafifu kuanzia 0 - 6.5. Watahiniwa hao walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mbinu za tafsiri hivyo kushindwa kueleza mbinu nne zinazoweza kutumika katika kutafsiri matini iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili kwenda lugha Kiingereza. Watahiniwa hao walikosa umahiri wa tafsiri mbalimbali zinazoweza kutumika kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine kama; tafsiri ya neno kwa neno, tafsiri sisisi, tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya kimawasiliano. Badala yake, baadhi walielezea dhima za lugha kama *kurahisisha mawasiliano, kujenga ushirikiano, kutambulisha jamii, kurithisha amali za jamii* na *kupatanisha jamii*. Wengine walielezea sababu za lugha ya Kiswahili kutumika katika shughuli mbalimbali kwa kutoa hoja kama; kuwa na *msamiati wa kutosha, kuwa na watumiaji wengi, kuwa na eneo kubwa, kuwa na wataalamu wengi, kuwa na machapisho* na *historia pana*; majibu ambayo ni kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa wa aina hiyo.

6. Kutafsiri ni kitendo cha kuhawilisha ujumbe, mawazo, taarifa au maarifa kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine kwa njia ya maandishi. Mtu ambaye anafanya kazi hii ya tafsiri lazima awe na taaluma hii ya tafsiri, lazima ajue lugha husu za matini anazoshughulika nazo, lazima ajue utamaduni wa lugha lengwa kabla ya kuifanyia tafsiri pia lazima ajue matukio mbalimbali yaani aendane na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Zifuatazo ni mbinu zinazomwezesha mfasiri huyo kuzitumia ili kufanya kazi hiyo ya tafsiri,

Ulinganifu wa matini, katika hatua hii mfasiri anatakiwa kulinganisha matini chanzi na matini lengwa ili ~~kusudi~~ aweze kuitafsiri matini chanzi kwa ~~ufahi~~ usahihi kama alivyolenga mwandishi wa matini chanzi kwenda kwa hadhira yake lengwa. Hivyo basi mfasiri anatakiwa afanye ulinganifu wake wa matini chanzi kwa matini lengwa kwa usahihi ili asikosee na wala asiongeze wala asipunguze msamiati ~~u~~ kwa hadhira ya lugha lengwa.

~~p~~ Kupima usili, katika hatua hii mwandishi anatakiwa kumpa mtu mwengine aisome kazi hiyo pasi na kuambiwa kama imefanyiwa tafsiri kusudi aweze kujua inaonekana vipi kama imeandikwa au imetafsiriwa. Mfasiri awe makini



6 kwa sababu kazi hiyo ya tafsiri inatakiwa isomeke vizuri yaani isionekane kama imefanyiwa tafsiri.
Kupima usomekaji, katika hatua hii mfasiri anatakiwa kupima kazi aliyoifanyia tafsiri kuwa inasomeka vipi je ~~vifatu~~ haina maana au inamaana iliyolengwa na mwandishi wa matini chanzi kwenda lugha lengwa. Mfasiri atakiwi kupunguza wala kuongeza maneno yake mwenyewe bali inatakiwa ayafasiri vyema yale yaliyoandikwa na mwandishi wa matini chanzi pia tafsiri hiyo isomeke vizuri.
Kupima uelewekaji, katika hatua hii mfasiri anatakiwa kupima uelewekaji wa kazi hiyo ya tafsiri kwa hadhira lengwa na aitathmini mwenyewe je! hadhira lengwa wa kazi hii ya tafsiri wataelewa kazi hii bila kupata shida au la lugha iliyotumika na msamiati yake inaeleweka kwa hadhira lengwa hiyo. Kazi hiyo inatakiwa kueleweka kama alivyolenga mwandishi wa matini chanzi kwenda kwa hadhira lengwa.
Hivyo basi, mfasiri baada ya kuhakikisha utimilifu na usawa wa hatua hizi kazi yake ya tafsiri itakuwa imekamilika vizuri sana na iko tayari kusomwa na hadhira lengwa. Hivyo ipo tayari kupelekwa kwa
6 Mwandishi wa lugha chanzi ili ajilidhishe na kazi yake.


**Kielelezo Na. 6.2**: Sampuli ya Jibu lisilo Sahihi katika Swali la 6

Katika Kielelezo Na. 6.2, mtahiniwa alielezea hatua mbalimbali za kutafsiri matini chanzi ili kuwa matini lengwa kwa kutoa hoja kama vile *ulinganifu wa matini, kupima uasili, kupima usomekaji*, na *kupima uelewekaji* kinyume cha matakwa ya swali.

### 2.1.2.3 Swali la 7: Kukua na Kuenea kwa Kiswahili

Swali hili lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili*, mada ndogo ya *Kukua na Kuenea kwa Kiswahili*. Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutathmini shughuli mbalimbali barani Afrika na ulimwenguni kwa ujumla zinazoendeshwa kwa lugha ya Kiswahili.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri sana ambapo watahiniwa 28,929 kati ya 29,184 walilijibu. Kati yao, watahiniwa 28,864 sawa na asilimia 99.78 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 7 hadi 20 kama inavyoonekana katika Chati Na. 6.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Katika Chati Na. 6, watahiniwa 65 (0.22%) walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5, watahiniwa 514 (1.78%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5 na watahiniwa 28,350 (98.00%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 12 hadi 20.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wengi (98.00%) walijibu vizuri swali hili na kupata alama kuanzia 12 hadi 20. Miongoni mwao, watahiniwa 10,111 sawa na asilimia 34.95 walipata alama za juu kuanzia 18 hadi 20 kutokana na kufafanua kwa

usahihi shughuli mbalimbali zinazofanywa barani Afrika na ulimwenguni kwa ujumla kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

Watahiniwa hao, walionesha kuwa na uelewa wa kutosha juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli mbalimbali barani Afrika na ulimwenguni, hivyo kuthibitisha matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa kutoa hoja sahihi kama vile: *kutumika kwenye shughuli za kielimu*, *kisiasa*, *kidiplomasia*, *kibiashara*, *kitalii*, na *shughuli za kidini.* Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama za juu.

7 Lugha ya kiswahili ni lugha ya taifa
kwa mataifa mbali mbali ya Afrika Mashariki
Mataifa hayo ni Tanzania, Kenya na uganda. Mara
baada ya uhuru Taifa la Tanzania lilitangaza kiswa
hili kuwa lugha ya taifa pia nchi nyingine kama
Kenya na uganda pia waalitangaza Kiswahili kuwa lugha
ya taifa ingawa kiswahili hakikupewa zaidi kipao
mbele katika nchi hizo za Kenya na Uganda. Kiswa
hili kama moja ya lugha ya kimataifa inatumika
katika shughuli mbali mbali kama vile elimu, Dini
Biashara na hata kwenye sanaa. Zifuatazo ni namna
Kiswahili inavyotumika katika shughuli mbali
mbali Barani Afrika na ulimwenguni

Matumizi ya kiswahili katika elimu
Kiswahili kama lugha mojawapo ya kimataifa ina
tumika katika shughuli mbali mbali za kielimu
hasa kama soma katika vyuo vikuu mbali mbali
Barani Afrika na ulimwenguni kote. Vyuo hivyo ni
kama vile Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam, chuo
kikuu cha Uingereza oxford na baadhi ya
vyuo vikuu vya Marekani na Afrika Kusini. pia
kwa hapa Tanzania kiswahili inatumika kama
lugha ya kufundishia kuanzia darasa la kwanza
mpaka la saba pia kama somo kwa shule za
Sekondari mpaka Chuo kikuu hivyo kiswahili ni
moja kati ya lugha ambayo inamchukua mchango mkubwa
katika elimu

Matumizi ya kiswahili katika vyombo
vya habari kiswahili pia inatumika katika shughuli
za kutoa habari. kazi inayofanywa na vyombo vya
habari kama vile ~~TBC, KBC,~~ BBC Redio na
televisheni vilivyoko ndani ya bara la Afrika na

7 ~~nchi~~ nje ya Bara la Afrika Mfano PBC KBC BBC VOA DW na Sauti ya Jamhuri ya ~~Kisalamu~~ Kislamu ya Asia vyombo hivi vinatoa habari na matangazo kwa lugha ya Kiswahili hasa habari. Hali hii ina changia kukua na kuenea kwa Kiswahili duniani kwa sababu vyombo hivi husikika duniani kote na watu wengi wanaweza kujifunza Kiswahili

Matumizi ya Kiswahili katika shughuli za Biashara Kiswahili ni miongoni mwa lugha mayotumika katika shughuli za kibiashara kwa hapa nchini na Barani Afrika lugha hii pia hutumika katika Biashara ya kimataifa hasa katika nchi ya China, Marekani, Afrika Kusini uingereza na Japani wafanya biashara wengi wa nchi hizo wanaowasiliana na wafanya biashara wa Tanzania kwa lugha ya Kiswahili pia Baadhi ya bidhaa machapisho yake yametafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili kitendo hicho hudhihirisha kuwa Kiswahili ni lugha maalumu inayotumika katika biashara

Matumizi ya Kiswahili katika mikutano mbali mbali ulimwenguni Kiswahili ni miongoni mwa lugha kuu ~~tano~~ kumi duniani lugha hii pia hutumika katika shughuli za mikutano mbali mbali mfano ~~Mkutano wa~~ ~~SADC~~ Mikutano ya Jumuiya ya nchi za Afrika Mashariki na kusini (SADC) pia Jumuiya ya nchi za Afrika Mashariki (EAC) pia mwaka 2010 Kiswahili pia ilianza kutumika katika mikutano ya umoja wa nchi za Afrika (AU) ambapo rais wa Tanzania kipindi hicho alipewa nafasi ya kuhutubia umoja huo kwa Kiswahili katika mkutano cha umoja wa mataifa Kiswahili pia kime pewa kipaumbele katika matumizi hivyo Kiswahili

7 kuwa moja ya lugha inayotumika katika mikutano ya kimataifa

Matumizi ya Kiswahili katika shughuli za kisanaa Kiswahili ni miongoni mwa lugha inayotumiwa sana katika sanaa kwa hapa Afrika hasa kwa Tanzania wapo wasanii wengi wa muziki wa Tanzania kama vile Alikiba, Diamond na Zuchu wasanii hawa wameandaa kazi zao nyingi na nyimbo kwa Kiswahili pia wameloushirikisha baadhi ya wasanii kutoka nchi mbali mbali duniani mfano Nigeria, Afrika Kusini, Ghana, Kongo DRC na Marekani hivyo Kiswahili ni moja ya lugha inayotumika katika sanaa.

Kiswahili kutumika kama lugha ya taifa katika nchi mbalimbali Afrika Lugha ya Kiswahili pia ni lugha ya taifa katika nchi mbali mbali barani Afrika mfano Tanzania Kenya Uganda na kama lugha rasmi katika nchi ya Burundi na Rwanda hivyo lugha hii hutumika ~~Kama~~ katika mawasiliano na shughuli zote rasmi katika nchi hizo.

Kwa ujumla Kiswahili ni miongoni mwa lugha inayokua kwa kasi duniani lakini lugha hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali inayotokana na wazawa wa lugha hii kwani wapo watu wengi hawathamini Kiswahili bali wanaona bora kutumia lugha zingine kama Kiingereza na Kiarabu hivyo huchangia kutokuenea kwa kasi ulimwenguni.

**Kielelezo 7.1**: Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 7

Katika Kielelezo Na. 7.1, mtahiniwa alitumia hoja sita sahihi zinazothibitisha kauli kuwa, "Lugha ya Kiswahili inatumika katika shughuli mbalimbali Barani Afrika na ulimwenguni kwa ujumla." Aidha, mtahiniwa alitumia mifano dhahiri ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika *elimu, biashara, vyombo vya habari, sanaa, mikutanoni* na *lugha ya taifa* na hivyo kupata alama za juu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 514 sawa na asilimia 1.78 waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 6.5 hadi 11.5. Majibu ya watahiniwa hao yalikuwa hayajitoshelezi kutokana na kutoa mifano ya shughuli zisizo sahihi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika bara la Afrika na duniani kwa ujumla. Baadhi ya watahiniwa walibainisha hoja sahihi lakini hawakufafanua kama ilivyostahili, hivyo walipata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja hoja zifuatazo: *Kiswahili kutumika katika kampeni za kisiasa, Kiswahili kutumika kama lugha ya taifa, Kiswahili kuteuliwa kama lugha ya kufundishia, kuanzishwa kwa asasi za Kiswahili, Kiswahili kutumika katika vyombo vya habari ingawa* hakufafanua namna shughuli hizo zinavyotumia lugha ya Kiswahili, na kupata alama za wastani.

Licha ya ufaulu mzuri katika swali hili, watahiniwa wachache (0.22%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kutokana na kukosa umahiri katika mada ya Maendeleo ya Kiswahili kwa ujumla. Watahiniwa hao, walishindwa kuthibitisha kwa mifano namna, "lugha ya Kiswahili inavyotumika katika shughuli mbalimbali barani Afrika na ulimwenguni kwa ujumla kwa kueleza mambo yasiyohusiana na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Baadhi yao walieleza dhima za lugha kama: *hurahisisha mawasiliano*, *hujenga ushirikiano*, *husaidia kukutanisha na kutambuana,* na *husaidia kurithisha amali za jamii;* majibu ambayo ni kinyume na mahitaji ya swali hili na hivyo walipata 0. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zifuatazo: *kuimarisha utawala, shughuli za kimahakama*, na *ujenzi wa miundombinu* ambapo ufafanuzi wake hakuonesha ni kwa namna gani shughuli hizo zinafanyika kwa kutumia lugha ya Kiswahili na eneo maalum la kijiografia halikubainishwa. Hali kadhalika, wapo watahiniwa walioeleza namna lahaja mbalimbali zilivyotumika katika kusanifisha lugha ya Kiswahili ambapo kiuhalisia shughuli hiyo ililenga katika kukuza Kiswahili ili kiweze kutumika na sio kujua asili ya lugha hiyo. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili.

7. , lugha ya kiswahili ni lugha inayo
tumiwa na waswahili lugha ya kiswa
hili inatumika katika shughuli mbalimbali
kwa Mfano shughuli za kibiashara, shughu
li za kisiasa, shughuli za kidiplomasia,
shughuli za kidini, shughuli za kielimu,
shughuli za kilimo barani Afrika na ulim
wenguni kwa ujumla zifuatazo ni sababu
za lugha ya Kiswahili kutumika katika
shughuli ~~za~~ mbalimbali

lugha ya kiswahili ina msamiati wa
kutosha; lugha ya kiswahili inatumika
katika shughuli ~~mbali~~ za kidini, za kieli
mu, za kibiashara, za kiutamaduni za
kidini barani Afrika na ulimwenguni
kwa ujumla kwa sababu lugha ya
Kiswahili ina msamiati wa kutosha.

. lugha ya kiswahili ina watumiaji wengi
lugha ya kiswahili inatumika katika shu
ghuli za kidini, kielimu, biashara, katika
vyombo vya habari, kilimo, ~~kidimplo~~ kidi
plomasia ~~kw~~ barani Afrika na ulimw
enguni kwa ujumla kwa sababu ina
watumiaji wengi

7. lugha ya kiswahili ina Machapisho mengi.
lugha ya kiswahili inatumika katika
shughuli mbalimbali barani Afrika na
ulimwenguni kwa ujumla katika shughuli
za kibiashara, kidiplomasia, kidini, kieli
mu, kilimo kwa sababu lugha ya kiswa
hili ina Machapisho mengi
lugha ya kiswahili ina mweneo
Mpana; lugha ya kiswahili inatumika ka
tika shughuli za biashara, elimu, kilimo
dini, shughuli za kidiplomasia kwa
sababu lugha ya kiswahili inachya
Mweneo mpana ndio maana, inatumika
katika shughuli mbalimbali barani Afrika
na ulimwenguni kwa ujumla.
lugha ya kiswahili ina wataalamu
wengi; lugha ya kiswahili inatumika
katika shughuli za biashara, elimu, kilimo,
dini, shughuli za kidiplomasia kwa saba
bu lugha ya kiswahili ina wataalamu
wengi ndio maana lugha ya kiswahili
inatumika katika shughuli mbalimbali ba
rani Afrika na ulimwenguni kwa ujumla.
lugha ya kiswahili ina historia pana
lugha ya kiswahili inatumika katika shu
ghuli za biashara, elimu, kilimo, dini,
shughuli za kidiplomasia kwa sababu lugha
ya kiswahili ina historia pana sana
ndio Maana lugha ya kiswahili ina
tumika katika shughuli mbalimbali barani
Afrika na ulimwenguni kwa ujumla.


**Kielelezo Na. 7.2:** Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 7

Katika Kielelezo Na. 7.2, mtahiniwa alielezea sababu mbalimbali zilizofanya lugha ya Kiswahili kuteuliwa na kutumika katika shughuli mbalimbali kutokana na kuwa na *msamiati wa kutosha*, *watumiaji wengi, mweneo mpana, wataalam wengi* na kuwa na *historia pana*; majibu ambayo ni kinyume na matakwa ya swali, hivyo kupata alama za chini.

#### 2.1.2.4 Swali la 8: Kukua na Kuenea kwa Kiswahili

Swali hili lilitoka katika mada ya Maendeleo ya Kiswahili, mada ndogo ya *Kukua na Kuenea kwa Kiswahili baada ya Uhuru*. Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu taasisi mbalimbali zilizosaidia kukuza na kueneza Kiswahili baada ya uhuru. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza majukumu ya TAKILUKI na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima katika kukuza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania, kwa kutumia hoja tatu kwa kila moja

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 9,120 (31.25) kati ya 29,184 waliofanya mtihani huu. Kati yao, watahiniwa 9,043 sawa na asilimia 99.16 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 7 hadi 20. Chati Na. 7 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na.** *7: Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8*

Katika Chati Na. 7, watahiniwa 77 (0.84%) walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5, watahiniwa 1,199 (13.15%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5 na watahiniwa 7,844 (86.01%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 12 hadi 20.

Uchambuzi unaonesha kuwa swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi ambapo asilimia (86.01%) walipata alama za juu kuanzia 12 hadi 20. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu taasisi mbalimbali

za kukuza na kueneza Kiswahili baada ya uhuru. Miongoni mwao, asilimia 11.61 sawa na watahiniwa 1,059 walitoa majibu toshelevu na kupata alama 18 hadi 20. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mchango wa TAKILUKI na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima katika kukuza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alieleza kwa usahihi majukumu ya TAKILUKI kama: *kutoa mafunzo na masomo ya Kiswahili kwa kiwango cha juu kwa watumishi wa serikali na viongozi wa chama ili kukuza Kiswahili*, *kuendesha mafunzo ya somo la Kiswahili na lugha za kigeni kwa wanafunzi wenyeji na wa kutoka nje*, na *kufanya utafiti wa lahaja na fasihi simulizi za Kiswahili*. Vilevile, alieleza majukumu ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa hoja kama: *kufundisha na kueneza Kiswahili kwa kutumia njia ya masomo ya jioni na kampeni za taifa za maendeleo*, *kusaidia wanafunzi kupata vitabu na majarida mbalimbali ya Kiswahili kutoka kwenye taasisi yao* na *kubuni maneno mbalimbali kukidhi haja ya msamiati na istilahi za Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima*. Aidha, watahiniwa hao walitoa utangulizi na hitimisho linaloendana na swali. Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu katika swali hili.


08 Majukumu ya TAKILUKI na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

TAKILUKI; Ni Taasisi ya Kiswahili na lugha za Kigeni nchini Zanzibar ambayo ilianzishwa mnamo mwaka 1997. Kwa sasa Taasisi hiyo imebadilishwa jina na kuitwa SKILUKI yaani Skuli ya Kiswahili na lugha za Kigeni Zanzibar; Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) ni taasisi inayojishughulisha na utoaji wa elimu kwa watu wazima wote nchini ambao hawakupata fursa ya kwenda shule. Yafuatayo ni majukumu ya TAKILUKI kama vile ifuatavyo;

Kufundisha lugha ya Kiswahili kwa Wageni wote nchini Zanzibar; Taasisi hii inajishughulisha na utoaji na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili Sanifu kwa Wageni wote wanaoenda kutembelea nchini ili kuweza kuwasaidia katika mawasiliano. Mfano; Watalii na watembezi kutoka Ulaya hufundishwa Kiswahili.

Kufanya Uchunguzi juu ya maneno na maana mbalimbali; Pia, Taasisi hii hufanya Uchunguzi juu ya maneno mapya yanayoibuka na kuzuka nchini ili yaweze kufanyiwa ~~Uchu~~ upatikanaji wa maana sahihi katika lugha ya Kiswahili.

Kuandaa Warsha na makongamano; Vilevile, Taasisi hii ina majukumu ya kuandaa na kutayarisha Warsha na makongamano mbalimbali ili kuweza kusaidia kusambaza na kukuza lugha hiyo ya Kiswahili.



Yafuatayo ni majukumu ya Taasisi ya Elimu ya Watu wazima (TEWW) katika kukuza lugha ya Kiswahili kama vile ifuatavyo;

Kutoa elimu kwa watu wazima; Taasisi hii ina majukumu ya kutoa elimu kwa watu wazima ambao hawakupata nafasi ya kwenda kusoma ili kuweza kupunguza idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika nchini pamoja na kupambana na ujinga.

Kutoa masomo kwa njia ya Posta; Pia, Taasisi hii hutoa masomo yake kwa njia ya posta hivyo kusaidia kukuza lugha ya Kiswahili kwa kusambaza nchi nzima. Mfano, maeneo ya vijijini hupata masomo hayo kwa njia ya Posta.

Kutoa masomo ya jioni; Kutokana na harakati za kupambana na maisha ili kujiingiza kipato. Taasisi - hujishughulisha na utoaji wa elimu kwa masomo ya jioni jambo linalosaidia kukuza lugha ya Kiswahili kwa watu wote nchini.

Hivyo basi; licha ya Taasisi hizi kuwa na majukumu na mchango mkubwa katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini, Taasisi hizo zinakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile uhaba wa fedha na muwamko mdogo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili jambo linalorudisha nyuma maendeleo yao.

**Kielelezo Na. 8.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 8

Hata hivyo, watahiniwa 1,199 sawa na asilimia 13.15 walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5. Watahiniwa hao waliweza kutoa hoja sahihi mbili hadi tatu kuhusu majukumu ya TAKILUKI na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima katika kukuza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Vilevile, baadhi ya watahiniwa walishindwa kutofautisha

majukumu ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na TAKILUKI. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza jukumu la *kuifanya lugha iwe na watumiaji wengi* ambalo halikuwa jukumu la Taasisi ya Elimu ya watu wazima bali yalikuwa ni mafanikio ya taasisi hiyo katika kutimiza majukumu yake hivyo, alipata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache sana (0.84%) waliojibu swali hili walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 6.5. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walishindwa kutoa hoja tatu sahihi kuhusu majukumu ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na TAKILUKI katika kukuza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Watahiniwa hao walionesha kukosa uelewa kuhusu taasisi hizo, hivyo kushindwa kueleza majukumu yake kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza majukumu yasiyo sahihi ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa hoja kama vile: *kutoa walimu watakaofundisha mashuleni*, *kutoa kamusi za matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili*, na *kuchapisha vitabu*, ambapo maelezo yake hayakujitosheleza. Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

8 TAKILUKI na Taasisi ya elimu ya Watu wazima ~~katika~~ ~~kwa~~ Ni taasisi ambazo zilianzishwa nchini kwa Madhumuni au Malengo Mbalimbali kwa ajili ya Watanzani a kwa kuanza na Taasisi ya elimu ya Watu Wazima hii ziwa na majukumu kama yafuatayo

Kuhakikisha Wanachapisha Majarida ya kutosha ili watumiaji Wasipate tabu katika ujifunzaji wao hivyo taasisi lihakikisha inaanda majarida ya kutosha kwa ajili ya kuhamasisha na pia kwa ajili ya kujua mee kwa watumiaji

Kuhakikisha kupata watadumu wa kutosha ili wawezeshe ikurahisishe ufundisha ji huo uwe wa urahisi na pia walimu hao wawe wamesomea taaluma hiyo kwa ajili ya kutumia mbinu bora za kufu ndishia Watu Wazima wanaohitaji elimu.

Kuhakisha kuwa Vifaa Vyote Vya kuji funzia Vinapatikana kwa urahisi mfano Vitabu vya kutosha ili watumiaji wawe ze kujifunza kwa urahisi na pia hii husaidia kwa kiasi au kiwango cha hali ya juu kwa kupata idadi kubwa ya Watu Wazima Wanaojua kusoma.

8 Takiluki pia ilikuwa ina majukumu ambayo yalisaidia kukuza Lugha ya Kiswahili nchi Tanzania

Kuhakikisha kuna kuwepo na Vifaa vya kutosha ili Wajifunzaji wajifunze kwa Urahisi lugha ya kiswahili vitabu ambavyo Vimechapishwa kwa ajili ya kujifunzia Lugha ya Kiswahili.

Kuhakikisha Sehemu ya kujifunzia wanafunzia wakapata sehemu aa nzuri ambayo ni rafiki kwa kujifunzia ni rahisi kuelewa hivyo Taasisi ilikuwa kitasha hilo

Hizo ndizo Taasisi ambazo zilikuwa na Majukumu ili kukuza lugha ya Kiswahili nchi lakini hivyo kwa taasisi fulani zilifanikiwa na kupata idadi kubwa ya watu wanaojua Lugha ya Kiswahili.

**Kielelezo Na. 8.2**: Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 8

Katika Kielelezo Na. 8.2, mtahiniwa alitoa hoja zisizo sahihi kuhusu majukumu ya TAKILUKI na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima katika kukuza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania kwa kuzingatia upatikanaji wa *vifaa, wataalam/walimu*, na *majarida* ili kufundishia lugha ya Kiswahili kinyume na matakwa ya swali, hivyo kupata alama za chini.

## 2.2 SEHEMU YA II: KISWAHILI KARATASI YA PILI

Karatasi ya pili imegawanyika katika sehemu A na B. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulikuwa kama ifuatavyo:


### 2.2.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne (4) yenye jumla ya alama 40, ambapo kila swali lilikuwa na alama 10. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu hii.

#### 2.2.1.1 Swali la 1: Maendeleo ya Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Fasihi Simulizi*, mada ndogo ya *Uhifadhi wa Kazi za Fasihi Simulizi*. Swali lilimtaka mtahiniwa kwa kutumia hoja tano kueleza ukweli wa kauli, "Uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi katika maandishi una changamoto nyingi".

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote (29,184) waliofanya mtihani huu. Ufaulu wa watahiniwa ulikuwa mzuri kwani asilimia 91.15 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Chati Na.8 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Katika Chati Na. 8, watahiniwa 2,292 (7.85%) walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 3, watahiniwa 4,219 (14.46%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5, na watahiniwa 22,673 (77.69%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 6 hadi 10.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha watahiniwa 22,673 sawa na asilimia 77.69 walijibu vizuri swali hili na kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Miongoni mwao, asilimia 32.03 walifanya vizuri zaidi na kupata alama za juu kuanzia 9 hadi 10. Ufaulu wao ulitokana na kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ndogo ya *Uhifadhi wa Kazi za Kifasihi*. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa waliweza kueleza ukweli wa kauli "Uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi katika maandishi una changamoto nyingi" kwa kutoa hoja sahihi kama vile: *kukosa vionjo vya masimulizi*, *kukosa ushirikishwaji wa hadhira*, *gharama nyingi za kuandika na kuchapa vitabu*, *hupoteza uwezo wa kupokea mabadiliko ya papo kwa papo*, na *huwa mali ya mtu binafsi*. Hata hivyo, kiwango cha ufaulu kati ya watahiniwa kilitegemea usahihi na maelezo kila mmoja. Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

1. (i) Huhitaji gharama kubwa - Fasihi Simulizi katika Maandishi huhitaji gharama ili kuweza kufikisha ujumbe kwa jamii Ikiwa ni pamoja na vifaa vitakavyotumika katika kuandika lakini pia nafasi ya kufikisha hayo maandishi au vitabu/majarida kwa watu mbalimbali.

(ii) Haiwezi kubadilika kulingana na wakati fasihi Simulizi katika Maandishi ikishaandikwa sio rahisi kurekebisha ujumbe kulingana na Mienendo ya jamii iliyopo kwa wakati

(iii) Huitaja Elimu na ujuzi wa kutosha; kazi ya fasihi Simulizi katika Maandishi Inahitaji Mtunzi awe na Elimu (ajue kusoma na kuandika) lakini pia Ujuzi wa kuweza kuwasilisha mawazo yake vizuri ili kila atakayesoma aweze kuelewa kwa urahisi.

(iv) Inaweza kutumiwa na watu wachache: Ukilinganisha fasihi simulizi na fasihi Simulizi katika Maandishi watu wanaojua kusoma na kuandika tu ndio wanaoweza kupata ujumbe uliokusudiwa kwa jamii.

(v) Huhitaji muda mrefu ili kufikisha ujumbe uliolengwa kwa jamii: fasihi Simulizi katika Maandishi huhitaji muda ili uweze kuandikwa vizuri na kupeleka ujumbe uliokusudiwa kwa jamii.


**Kielelezo Na. 9.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 1

Katika Kielelezo Na. 9.1, mtahiniwa alielezea kwa usahihi changamoto tano zinazokabili uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi katika maandishi kwa kutumia mifano iliyokidhi matakwa ya swali.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa asilimia 14.46 walijibu swali hili na kupata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5. Watahiniwa hao

walishindwa kuelezea kikamilifu changamoto tano za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi katika maandishi. Katika kundi hili, wapo watahiniwa ambao walieleza hoja mbili hadi tatu pekee na wengine walitoa ufafanuzi usiojitosheleza kwa hoja walizotoa hivyo, walipata alama za wastani.

Uchambuzi zaidi wa majibu unaonesha kuwa, watahiniwa 2,292 sawa na asilimia 7.85 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo juu ya mada ya uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi, hususan katika maandishi. Kati yao, watahiniwa 472 walipata 0 kutokana na kushindwa kabisa kueleza hoja hata moja kati ya hoja 5 zilizotakiwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja na maelezo yasiyo sahihi kama vile: *tatizo la uchapaji*, *tatizo la umma unaoandikiwa*, *tatizo la wahakiki*, *uhaba wa waandishi wa kazi za fasihi*, na *maendeleo ya sayansi na* teknolojia. Baadhi ya watahiniwa walionesha tofauti kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi na wengine walieleza changamoto zinazoikabili fasihi andishi kwa hoja kama vile *uhaba wa fedha, uhaba wa wataalam* na *uhaba wa vifaa vya kisasa kama vile kompyuta*; majibu ambayo ni kinyume cha matakwa ya swali hili. Watahiniwa hao walitakiwa kueleza changamoto tano za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi katika maandishi kama vile *kukosa vionjo vya masimulizi*, *kukosa ushirikishwaji wa hadhira*, *gharama nyingi za kuandika na kuchapa vitabu*, *hupoteza uwezo wa kupokea mabadiliko ya papo kwa pao*, na *huwa mali ya mtu binafsi*. Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili na kupata 0.



1. Fasihi simulizi ni aina
ya fasihi ambayo hutumia
wahusika wasiokuwa na kufanikisha
kazi ya sanaa. Fasihi Simulizi
huhifadhiwa kichwani hivyo ni
rahisi kusahau. Uhifadhi wa
kazi za fasihi katika maandishi
una changamoto nyingi, changamoto hizo ni
Makosa ya kimatamshi
badala ya kuandika sa, mtahiniwa
kuandika tha, hii hupunguza
ubora wa kazi ya fasihi
Makosa ya kimtindo.
kazi ya fasihi andishi hufuata
mtindo kupitia kusimuliwa ni
vigumu kujua itaandikwa mtindo upi
kama ni wa, mtindo wa swali.
Makosa ya kimuundo ni
vigumu kujua ni mtindo upi utatumika
kupitia kusimuliwa
Makosa ya kimaana.
kupitia masimulizi na kuweka
kwenye maandishi ni vigumu
kueleza msimuliaji alikuwa anataka
kueleza kitu gani

**Kielelezo Na. 9.2:** Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 1.

Katika Kielelezo Na. 9.2, mtahiniwa alibainisha dhana zinazohusu aina mbalimbali za makosa ya kisarufi katika lugha kinyume na mahitaji halisi ya swali hili ambapo alitakiwa kueleza changamoto za uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi katika maandishi.

#### 2.2.1.2 Swali la 2: Fasihi kwa Ujumla

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi kwa Ujumla*, mada ndogo ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Swali lililenga kutathmini hasara nne za uhakiki kwa mtunzi wa kazi za fasihi. Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua kauli "Wahakiki wa zama hizi hulenga kujitajirisha wao tu wala si kwa faida ya mtunzi asilia."

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote (29,184) waliofanya mtihani huu. Swali hili lilijibiwa vizuri sana ambapo watahiniwa 21,803 sawa na asilimia 74.70 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Jedwali Na. 3 linaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

**Jedwali Na. 3: Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa**

| Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0 – 6.5 | 7,381 | 25.29 |
| 7 - 11.5 | 8,164 | 27.97 |
| 12 -20 | 13,639 | 46.73 |

Katika Jedwali Na. 3, watahiniwa 7,381 (25.29%) walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 3, watahiniwa 8,164 (27.97%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5 na watahiniwa 13,639 (46.73%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 6 hadi 10.

Uchambuzi wa takwimu za ufaulu unaonesha kuwa, watahiniwa 13,639 sawa na asilimia 46.73 walijibu vizuri swali hili na kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Miongoni mwao, watahiniwa 5,564 sawa na asilimia 19.07 walitoa majibu sahihi zaidi na kupata alama za juu 8 hadi 10. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya nadharia ya uhakiki wa kazi za fasihi, hivyo kueleza kwa usahihi hasara za uhakiki kwa mtunzi wa kazi za fasihi. Watahiniwa hao waliweza kutumia hoja nne sahihi na mifano katika kutathmini hasara za uhakiki kwa hoja kama vile *mhakiki kuwa mnyonyaji wa kazi ya mtunzi*, *mhakiki hupata umaarufu zaidi kuliko* mtunzi, *mhakiki hupata fedha nyingi zaidi kuliko mtunzi*, *mawazo ya mhakiki hutegemewa zaidi kuliko ya mtunzi, uhakiki huweza kuua uhuru wa mwandishi*, na

*mhakiki huweza kuhatarisha maisha ya mtunzi wa kazi ya fasihi kuwa huweka wazi yaliyojadiliwa.* Kielelezo Na.10.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


2. Zifuatazo ni hasara za uhakiki kwa mtunzi wa kazi ya fasihi
(i) Mtunzi wa kazi ya fasihi hutakiwa kutoa gharama nyingi ili kazi yake iweze kuhakikiwa.
- Wahakiki wengi wamekua wakitumia taaluma ya uhakiki kama chanzo cha mpato hivyo huwataka watunzi wa kazi za fasihi kulipa fedha nyingi ili wahakikiwe.
(ii) Uhakiki huweza kupelekea kazi ya mtunzi wa kazi ya fasihi kufungiwa.
- kutokana na taaluma ya uhakiki huweza kupelekea kazi ya fasihi kufungiwa kwa sababu tu haijakidhi ugezu hali ambayo ni hasara kwa mtunzi ambaye ametumia fedha nyingi kuiandaa.
(iii) Uhakiki huweza kuchangia kupungua kwa ubora wa kazi ya fasihi.
- taaluma ya uhakiki kwa namna moja ama nyingine inaweza kuchangia ubora wa kazi ya fasihi kupingika kwa mhakiki kumuamuru mtunzi kupunguza baadh. ya upangele.
(iv) Uhakiki huweza kupelekea mtunzi wa kazi ya fasihi kukosa uhuru wake.
- kutokana na kazi ya fasihi kukaguliwa husababisha mtunzi huyo kushindwa kuandika baadhi ya vitu ambayo wahakiki hawataki uwepo hali inayopunguza ubora wa kazi ya fasihi.

**Kielelezo Na. 10.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 2

Katika Kielelezo Na. 10.1 mtahiniwa alijibu vizuri swali hili kwa kueleza hasara za uhakiki kwa mtunzi wa kazi za fasihi kwa usahihi kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nadharia ya uhakiki.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 8,164 (27.97%) waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5. Katika kujibu swali hili, baadhi ya watahiniwa walirudia hoja hivyo kuwa na hoja chache, wengine walitoa hoja bila ufafanuzi unaojitosheleza. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea faida ya mhakiki kama vile kupata fedha/ajira*, kupata umaarufu, kuhakikisha jamii inapata kazi iliyo bora n.k* hoja ambazo kiuhalisia zinamlenga mhakiki zaidi kuliko mtunzi, hivyo alipata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa wengine (25.29%) waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3. Miongoni mwa sababu zilizoathiri ufaulu wa watahiniwa katika kundi hili ni kukosa umahiri kuhusu nadharia ya uhakiki, hivyo kushindwa kueleza hasara za uhakiki kwa mtunzi wa kazi za fasihi. Uchambuzi umebainisha kuwa, baadhi ya watahiniwa walijadili fani na maudhui katika kazi mbalimbali za fasihi kama vile *dhamira mbalimbali*, *wahusika*, na *matumizi ya lugha* kinyume cha matakwa ya swali. Pia, watahiniwa wengine walielezea hasara za udhamini wa kazi za fasihi kama vile *kuua uhuru wa mtunzi, kazi ya mtunzi kuwa mali ya mdhamini*, *kazi ya mtunzi huamuliwa na mdhamini* na *kuzuka kwa riwaya pendwa*; majibu ambayo ni kinyume na matakwa ya swali. Kwa ujumla watahiniwa hao walitakiwa kueleza hasara za uhakiki kwa mtunzi wa kazi za fasihi kama vile *mhakiki kuwa mnyonyaji wa kazi ya mtunzi*, *mhakiki hupata umaarufu zaidi kuliko* mtunzi, *mhakiki hupata fedha nyingi zaidi kuliko mtunzi*, *mawazo ya mhakiki hutegemewa zaidi kuliko ya mtunzi, uhakiki huweza kuua uhuru wa mwandishi* na *mhakiki huweza kuhatarisha maisha ya mtunzi wa kazi ya fasihi kwa kuwa huweka wazi yaliyojadiliwa.* Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili, hivyo kupata alama hafifu.



02. Mhakiki ni mtu anayechambua
vipengele vya fani na maudhui kwenye ka
zi ya fasihi. Zifuatazo ni hasara za uha
kiki kwa mtunzi wa kazi ya fasihi.
Kushindwa kumshauri mwandishi af
anye kazi bora, hii ni hasara mojawapo tunaon
a waandishi na watunzi huandika kazi zao
ambazo hazifai kwa sababu ya rushwa ina
yofanyika.
Kuchochea rushwa, wahakiki wa dham
hizi hushindwa kuhakiki kazi kwa usahihi k
wa sababu ya rushwa inayofanyika na wana
fijali wao kama wao.
Kushindwa kufikisha ujumbe unaotaki
wa kwa jamii kwa sababu ya falsafa inaku
wa haieleweki kwa wanajamii pale wanaposo
ma kazi hizo.
Kuzuka kwa riwaya pendwa, pia
wanaongeza fasihi pendwa ambazo hazina
umuhimu wowote kwa jamii ya sasa na
kuvunja maadili mema kwa jamii.
Kuchochea matabaka, kwa saba
bu mhakiki atakuwa kivyake na mtunzi
atakuwa anafanya kazi yake peke yake am
bapo inaleta matabaka kwa jamii.

**Kielelezo Na. 10.2:** Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 2

Katika Kielelezo Na. 10.2 mtahiniwa alieleza baadhi ya athari za udhamini hususani *kuchochea rushwa, kuzuka kwa riwaya pendwa na kuchochea matabaka* kinyume cha matakwa ya swali.

### 2.2.1.3 Swali la 3: Fasihi kwa Ujumla

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi kwa Ujumla*, katika mada ndogo ya *Nadharia ya Fasihi*. Swali lililenga kupima uchambuzi na lilimtaka mtahiniwa kuchambua tofauti tano kati ya tenzi na mashairi.


Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote waliofanya mtihani. Ufaulu wa watahiniwa ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 19,367 sawa na asilimia 66.37 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Jedwali Na. 4 linaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

**Jedwali Na. 4: Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa**

| Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0 – 3 | 9,818 | 33.64 |
| 3.5 - 5.5 | 7,292 | 24.99 |
| 6 -10 | 12,075 | 41.78 |

Katika Jedwali Na. 4, watahiniwa 9,818 (33.64%) walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 3, watahiniwa 7,292 (24.99%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 3.5 walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama hadi 5.5 na watahiniwa 12,075 (41.78%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6 hadi 10.

Takwimu za ufaulu zinaonesha kuwa watahiniwa 12,075 sawa na asilimia 41.78 walifaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Kati yao, watahiniwa 5,535 sawa na asilimia 19.7 walipata alama za juu kuanzia 8 hadi 10. Watahiniwa hao waliweza kuchambua kwa usahihi tofauti tano kati ya tenzi na mashairi kama vipera vya ushairi wa fasihi simulizi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichambua vizuri tofauti zote tano zilizopo kati ya tenzi na mashairi kwa hoja kama vile *tenzi ni ndefu na zina beti nyingi wakati mashairi yana beti chache*, *tenzi zote huelezea tukio au dhamira moja tu wakati mashairi kwa kila shairi moja huweza kuwa na dhamira zaidi ya* moja, *tenzi zina vina bahari mwishoni lakini mashairi yana vina vya kati na mwisho*; *kimuundo - tenzi huwa na kipande kimoja tu wakati mashairi huwa na vipande zaidi ya kimoja*, na *tenzi hufuata kanuni za kimapokeo lakini mashairi huweza kufuata kanuni za kimapokeo au mamboleo*. Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyechambua kwa usahihi tofauti zote tano kati ya tenzi na mashairi kwa kukidhi matakwa ya swali hili.



3. i) Tofauti ya Urefu, kwa kawaida tenzi ni-
ndefu sana kuliko Hata Mashairi, kwani -
tenzi inaweza kuwa na beti mia moja Lakini -
Mashairi siyo marefu na hayana beti nyingi.

ii) Tofauti ya Mizani, Pia Tenzi huwa na mizani-
nane tu Lakini Mashairi huwa na mizani -
kumi na sita kwa kila Mstari.

iii) Vina, Tenzi, ina vina vya mwisho tu Lakini -
Mashairi huwa na vina vya kati na vya -
Mwisho mwisho

iii) Tofauti ya vina; Tenzi huwa na vina
vya mwisho tu Lakini mashairi yana
vya kati na vina vya mwisho.

iv) Tofauti ya Muundo, Tenzi huundwa na -
Muundo wa Ukwapi yaani ina upande mmoja -
tu Lakini Mashairi ya muundo wa Ukwapi na
Utao, yaani upande wa kulia huitwa utao na -
upande wa kushoto huitwa Ukwapi.


v) Tofauti ya Mtindo; Pia Mashairi huwa na -
Mtindo wa Kimapokeo na kisasa, kukuna baadhi ya -
Mashairi yanayo fuata ulinganifu wa Vina na Mizani -
to na mengine hayafuati mtindo huo. Lakini -
Tenzi haina [illegible] Mtindo wa kisasa, kwani -
ni lazima tenzi iwe na mizani nane na vina vyote
vya mwisho vifanane kwa kila Ubeti.

**Kielelezo Na.11.1**: Sampuli ya Majibu sahihi katika Swali la 3

Katika Kielelezo Na.11.1, mtahiniwa alichambua kwa usahihi tofauti zote tano kati ya tenzi na mashairi kwa kuzingatia *urefu, mizani, vina, muundo* na *mtindo.*

Kadhalika, watahiniwa 7,292 sawa na asilimia 24.99 walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5. Uchambuzi wa majibu yao unaonesha kuwa baadhi ya watahiniwa walikosa uelewa wa kutosha juu ya tenzi na mashairi kama vipera vya utanzu wa ushairi, hivyo kuweza kuchambua kwa usahihi baadhi ya tofauti na kushindwa kuchambua kwa usahihi tofauti nyingine. Vilevile, watahiniwa wengine waliweza kuchambua tofauti za *vina*, *mizani*, na *muundo* vinavyobainika katika mashairi na tenzi lakini walishindwa kuonesha tofauti ya *msuko wa matukio*, *urefu*, na *mtindo* vilivyopo katika mashairi na tenzi. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alichambua kwa usahihi tofauti mbili kama vile *tenzi huwa na vina vya mwisho pekee lakini mashairi (kimapokeo) yana vina vya kati na vya mwisho*, *tenzi huwa na mizani nane wakati mashairi huwa na mizani kumi na sita*, hivyo kupata alama za wastani.
.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 9,818 sawa na asilimia 33.64 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3. Sababu za ufaulu hafifu kwa watahiniwa hao ni pamoja na watahiniwa kutoa majibu yasiyojitosheleza katika kuchambua tofauti zilizopo kati ya tenzi na mashairi vinavyojibainisha katika urefu, msuko wa matukio, vina, mizani, muundo na mtindo. Pia wengine walionesha kutokuelewa matakwa ya swali hili hatimaye kuandika mambo mseto yasiyokuwa na uhusiano na *tenzi* na *mashairi*. Kutokana na kukosa umahiri huo, baadhi ya watahiniwa walichambua vipengele vya maudhui na fani katika kazi za fasihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichambua vipengele vya fani kwa hoja kama vile *muundo*, *mtindo*, *matumizi ya lugha*, *wahusika*, na *mandhari*. Wengine walitunga beti za mashairi na tenzi zenye ujumbe mbalimbali badala ya kuchambua tofauti tano kati ya tenzi na mashairi kama swali lilivyotaka. Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa wa aina hiyo.


3. Tenzi na Mashairi yote ni sanaa za
ushairi ambazo huwa na lengo la kufundisha na
kuonya jamii juu ya mambo yanayoikumba
jamii hata hivyo licha ya kuwa na lengo moja
lakini bado vinatofautiana kama ifuatavyo
Muundo, Tenzi na mashairi
hutofautiana katika kipengele cha muundo kuwa
mashairi yanakuwa na muundo wa tarbia, vina
na mizani lakini tenzi yenyewe ina kuwa ni
nusu mstari pia hakuna upande wa pia
kuna vina tu na hakuna mizani
Mtindo, vilevile tenzi na
mashairi hutofautiana katika kipengele
cha mtindo mtindo ya tenzi huwa ni
tofauti na mtindo ya Mashairi Mashairi
huweza kuandikwa kwa Mtindo ya kwasa
na kimapokeo lakini tenzi mtindo ndo ule
ule haubadiliki
Matumizi ya lugha vile
vile katika matumizi ya lugha tenzi hutumia
ya lugha ya kisanaa lakini sio sana ukilinganisha
sha na Mashairi yenyewe hutumia lugha
ya kisanaa, picha, misemo na misemo
lakini tenzi hutumia lugha pambanuzi
ya wazi
Wahusika, pia huwa
tofauti kwenye wahusika Mashairi
huweza kuwatumia kwa wahusika fulani
wanafunzi, wafanyakazi na viongozi
lakini tenzi hutumika kwa wote
wanaweza kuhusika.


**Kielelezo Na. 11.2**: Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 3

Katika Kielelezo Na.11.2 mtahiniwa alibainisha vipengele vya fani vinavyotumika katika uhakiki wa kazi za fasihi kinyume na matakwa ya swali, hivyo alipata alama 0.

#### 2.2.1.4 Swali la 4: Usanifu wa Maandishi

Swali lilikuwa mahsusi kupima uchambuzi na lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, mada ndogo ya *Usanifu wa Maandishi.* Swali lilimtaka mtahiniwa kusoma matini ya nathari kisha kubainisha vipengele vya kifani.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 29,184 sawa na asilimia 100 ya wote waliofanya mtihani. Hili ni swali lililojibiwa vizuri sana na idadi kubwa ya watahiniwa ambapo watahiniwa 23,851 (95.43%) walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Chati Na. 9 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 9***: Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 4*

Katika Chati Na. 9, watahiniwa 1,333 (4.57%) walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 3, watahiniwa 7,859 (26.93%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 3.5 hadi 5.5 na watahiniwa 19,992 (68.50%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6 hadi 10.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wengi (19,992) sawa na asilimia 68.50 walifaulu kwa kiwango kizuri na kupata alama kati ya 6 hadi 10. Miongoni mwao, watahiniwa 4,838 sawa na asilimia 16.58 walijibu swali hili vizuri zaidi na kupata alama za juu kati ya 8 hadi 10. Watahiniwa hao, walionesha kuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ndogo ya *Usanifu wa Maandishi* hivyo kuchambua kwa usahihi vipengele vyote sita vya kifani ambavyo ni


*muundo, mtindo, wahusika, mandhari, matumizi ya lugha*, na *taswira/picha* katika matini waliyopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu vizuri swali hili kwa kuchambua kwa usahihi vipengele sita vya fani vilivyounda matini aliyopewa kwa hoja kama vile *mtindo, muundo, wahusika, mandhari, matumizi ya lugha*, na *taswira/picha* pamoja na kutoa mifano kama ilivyojitokeza kwenye matini aliyopewa. Kielelezo Na.12.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama za juu.

4. (a) Muundo.. - ni mpangilio wa visa na matukio.
mwandishi ametumia muundo wa moja kwa moja kwani ameanza kwa kutusimulia maisha ya Tisade baada ya kufiwa na baba yake mzazi hadi ambapo Tisade anawaza na kufikiria kulipiza kisasi kwa aliyemuua baba yake mzazi.

(b) Mtindo.
ni upekee ambao mwandishi anautumia kutofautisha kazi yake na kazi ya mwandishi mwingine.
Mwandishi ametumia mtindo wa masimulizi katika kazi hii kwani hajahusisha matumizi yoyote ya lugha ya majibizano (dayalojia) au nyimbo ametumia masimulizi

(c) Wahusika
ni watu, vitu, wanyama, viumbe hai na visivyo hai ambavyo mwandishi huvitumia ili kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa.
- Rukendakenda
- Tisade
- Raina
- Kazimoto
- Mchumba wake Raina.

(d) Mandhari
ni mahali au sehemu ambapo shughuli au kazi za fasihi hufanyika. Zipo aina mbili za mandhari ambayo ni ya kubuni na mandhari halisi. Habari hii imetumia mandhari halisi ya nyumbani ambapo. Tisade anaonekana akiwa ameketi sebuleni ameketi chumbani pia anaoneshwa akiwa jikoni.



4. (e) Matumizi ya lugha-
ni namna ambayo mwandishi anatumia lugha mbalimbali kufikisha ujumbe kwa jamii yake.
Mwandishi ametumia lugha mbalimbali za kisanaa.
(i) Takriri
tamathali ya semi ambayo neno hujirudia rudia, mfano: Kisasi! Kisasi!
(ii) Tashibiha
tamathali ya semi ambayo inatumia kiunganishi katika kulinganisha maneno
mfano: Alikuwa amechanua kama ua la waridi
(iii) Mdokezo
ni hali ya kutamka neno au sentensi bila kulimalizia
mfano Lakini - - - .siyo heshima - - - - - - -
(iv) Tashihisi
ni hali ya kuvipa vitu visivyohai uwezo wa kutenda kama viumbe hai-
mfano. Moyo ukachukua mapigo ya nguvu haraka sana.

**Kielelezo Na.12.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 4

Katika Kielelezo Na.12.1, mtahiniwa alibainisha kwa usahihi vipengele sita vya kifani katika matini ya nathari. Aidha, mtahiniwa huyo alionesha umahiri wa hali ya juu kwani alielezea maana ya kipengele husika na namna kilivyotumika katika matini kwa usahihi.

Takwimu zinaonesha kuwa, watahiniwa 7,859 sawa na asilimia 26.93 waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5 kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kuhusu mbinu za kifani zilizotumika katika matini waliyopewa. Watahiniwa hao walichambua kwa usahihi baadhi ya vipengele vya kifani na kushindwa vingine kwa kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Usanifu wa Maandishi*, hivyo walipata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa 1,333 sawa na asilimia 4.57 walikuwa na ufaulu hafifu katika swali hili kutokana na kukosa umahiri wa kuchambua mbinu za kifani zilizotumika katika matini waliyopewa. Baadhi yao walishindwa kuchambua kipengele hata kimoja kuhusu mbinu za kifani katika matini husika. Wengine waliweza kubainisha vipengele vichache kati ya *mandhari, wahusika, muundo, mtindo*, na *matumizi ya lugha* lakini walishindwa kutoa mifano sahihi kwa kila kipengele,

hivyo kupata alama za chini. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kwa usahihi majina ya vipengele kama vile *wahusika, mandhari, matumizi ya lugha, mtindo*, na *muundo* lakini alishindwa kuvibainisha katika matini aliyopewa. Mtahiniwa mwingine alichambua tamathali za semi peke yake kama vile *tashihisi*, *tashtiti*, *tashibiha*, *madokezo*, *tafsida*, na *mubalagha* ambayo ni mbinu nyingine ya kisanaa katika kipengele cha matumizi ya lugha, hivyo kuwa na alama pungufu. Pia, wapo watahiniwa waliochanganya vipengele vya fani na vipengele vya maudhui kwa kubainisha vipengele kama vile *ujumbe, dhamira*, na *falsafa* kinyume cha matakwa ya swali. Kielelezo Na. 12.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili na hivyo alipata alama hafifu.

4. Vipengele vya fani
i. Matumizi ya misemo.
mfano. Usiue.

Matumizi ya Takriri - kurudia rudia
mfano. kisasi, kisasi

Matumizi ya Tanakali sauti.
mf. Loo! Mama wee! La haula!

Tashibiha
Alirudi kitandani na kujitupia kimya.

Tashihisi

Matumizi ya Mjalizo
Lakini ... hapana ... siyo heshima ...

Methali.

Nahau

**Kielelezo Na.12.2:** Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 4

Katika Kielelezo Na. 12.2**,** mtahiniwa alionesha vipengele vya matumizi ya lugha badala ya kuchambua kwa mifano vipengele sita vya kifani vilivyounda matini aliyopewa ambavyo ni *muundo, mtindo, wahusika, mandhari, matumizi ya lugha*, na *taswira/picha*.


### 2.2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAREFU

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne (4) ya insha ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu. Swali la sita lilikuwa la lazima. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 60 na kila swali lilikuwa na alama 20.

#### 2.2.2.1 Swali la 5: Uhakiki wa Ushairi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi*. Swali lilimtaka mtahiniwa kutetea hoja kwamba, "Usaliti ni sumu ya maendeleo kwa jamii" na kuonesha jinsi wasanii wanavyopinga usaliti huo kwa kutoa hoja tatu kwa kila diwani katika diwani mbili alizosoma.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wachache zaidi ikilinganishwa na maswali mengine ya kuchagua katika karatasi hii ambapo watahiniwa 5,609 (19.2%) pekee ndio waliolijibu. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo watahiniwa 5,028 sawa na asilimia 89.64 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 20. Chati Na. 10 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia katika swali la 5.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5*

Katika Chati Na. 10, watahiniwa 581 (10.36%) walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5, watahiniwa 1,056 (18.83%) walifaulu

kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5 na watahiniwa 39,72 (70.81%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 12 hadi 20.

Uchambuzi wa majibu unaonesha kuwa watahiniwa 3,972 sawa na asilimia 70.81 walijibu vizuri na kupata alama kuanzia 12 hadi 20. Miongoni mwao watahiniwa 957 sawa na asilimia 17.06 walifaulu vizuri zaidi kwa kupata alama za juu kuanzia 18 hadi 20. Ufaulu mzuri wa watahiniwa ulitokana na kuwa na uelewa wa kutosha wa mashairi katika diwani teule, hivyo kukidhi matakwa ya swali hili ipasavyo. Watahiniwa hao waliweza kutumia mifano kutoka katika diwani mbili walizosoma kujenga hoja kwamba, *Usaliti ni sumu ya maendeleo kwa jamii.* Watahiniwa hao waliweza kuonesha jinsi wasanii walivyopinga usaliti huo kwa kutoa hoja tatu kwa kila diwani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia diwani ya "Chungu Tamu" kutoa hoja kama vile *usaliti katika makubaliano kati ya mtu na watu au kikundi fulani* kutoka katika shairi la "Chatu na Kuku", *usaliti katika ndoa* katika shairi la "Fikra za Waungwana" na *Usaliti wa viongozi dhidi ya tabaka tawaliwa* katika shairi la "Samaki Mtungoni." Vivyo hivyo, katika diwani ya "Kimbunga" mtahiniwa mwingine alitoa hoja sahihi zinazoonesha jinsi msanii alivyopinga usaliti kama vile *usaliti wa tabaka tawala kwa tabaka tawaliwa* katika shairi la "Kibwangai", *usaliti wa kiutamaduni* katika shairi la "Vijana wa Zanzibar" na *usaliti wa kimapenzi* katika shairi la "Sitaki." Watahiniwa hao waliweza kutoa mifano dhahiri ya mashairi kutoka katika diwani teule. Pia, walikuwa na utangulizi na hitimisho zuri linaloendana na swali. Hata hivyo, tofauti ya alama kati ya watahiniwa hao, ilitegemea usahihi wa mifano waliyotoa kutoka katika diwani teule. Kielelezo Na. 13.1 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

5. Usaliti:- Ni hali ya mtu au watu kwenda kinyume na makubaliano ambayo waliweka kati yao. Usaliti ni kitu kibaya katika jamii na ni sumu ya maendeleo kwa jamii yetu. Kwa kutumia diwani ya KIMBUNGA iliyoandikwa na HAJI GORA na diwani ya FUNGATE YA UHURU iliyoandikwa na MOHAMED S. KHATIBU tunaona jinsi wasanii walivyopinga Usaliti katika jamii zao. Kwa kuanza na diwani ya KIMBUNGA hoja zifuatazo zinaonyesha jinsi wasanii walivyopinga Usaliti:-

Amepinga Usaliti kwa Viongozi wabaya dhidi ya wananchi wao. Msanii ametumia shairi la KIMBUNGA kuonyesha dai hilo la Uongozi mbaya dhidi ya wananchi wao anaposema,

"Kimbunga mji wa siyu, kilichowahi kufika,
Si kwa yule wala huyu, ilikuwa patashika,
Kimeng'oa mibuyu, minazi kuinusurika,
Nyoyo zilifadhaika"

Hata katika jamii zetu wapo viongozi ambao ni wabaya na ni wasaliti kwa wananchi wao. Mfano ni Iddi Amini Dada wa Uganda.
Ujumbe:- Watu wanapaswa kuacha Usaliti pale wanapopata Uongozi bali waendelee kuwasaidia wananchi wao ili kujenga jamii bora.

Amepinga Usaliti wa Unyonyaji wa nchi zilizoendelea kwa nchi zisizoendelea. Msanii ametumia shairi la CHUWI kupinga Usaliti huo pale anaposema,

5 "Ambao ni matajiri pale anapowafikia,
Huweza kujisitiri, salama kujipatia,
Walokuwa mafakiri huzidi kuwaonea,
Huyu ndiye Chui gani?

Hata katika jamii zetu Usaliti kati ya nchi zilizoendelea na zisizoendelea upo na kusababisha umaskini kwa nchi zisizoendelea. Mfano: kati ya Afika na Marekani au Ulaya. Ujumbe: Nchi ambazo bado hazijaendelea zinapaswa kupingana na suala hili kwani huzidisha Unyonyaji wa mali za nchi ambazo bado hazijaendelea.

Amepinga usaliti wa rushwa kwa wenye navyo na wasio navyo: Msanii amepinga suala hili la Usaliti kwa wenye navyo na wasionavyo kupitia Shairi la RUSHWA anaposema,

"Rushwa kajenga kambi,
Afanya kila vitimbi, Mkaidi hashindiki
Tumchimbieni handaki, Rushwa tukamzikeni

Hata katika jamii zetu Upo Usaliti kati ya Wenye navyo na wasio navyo kwani hutumia mali zao kwa njia ya rushwa na kuwanyonya wasionavyo. Mfano ni matrafiki barabarani na kwenye huduma za Afya. Ujumbe watu wanapaswa kuachana na Usaliti huu kwani hurudisha nyuma maendeleo.

**Kielelezo Na.13.1*:*** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 5.

Katika Kielelezo Na. 13.1, mtahiniwa alifafanua kwa usahihi jinsi wasanii walivyopinga usaliti kwa kutoa hoja stahiki katika diwani ya "Kimbunga" kwa kutumia mifano sahihi ya mashairi na kuandika utangulizi mzuri ulioendana na swali hili na kupata alama za juu.

Pamoja na ufaulu mzuri wa watahiniwa, baadhi ya watahiniwa (18.83%) walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama kati ya 7 hadi 11.5 kwa kuwa walitoa majibu yasiyojitosheleza katika kutetea hoja kuwa, *usaliti ni sumu ya maendeleo kwa jamii* na kuonesha jinsi wasanii walivyopinga usaliti huo. Baadhi ya watahiniwa walitoa hoja sahihi za mashairi lakini walishindwa kutetea baadhi ya hoja zao kikamilifu. Aidha, wengine hawakuandika utangulizi wala hitimisho, hivyo kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika diwani ya "Fungate ya Uhuru" alionesha usaliti unaopingwa na msanii kuwa ni kama vile *tabaka tawaliwa dhidi ya viongozi, nyumba za ibada*, *na waafrika dhidi ya ukoloni* lakini alitaja mashairi yasiyowiana na hoja hizo, hivyo akapata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 581 sawa na asilimia 10.36 walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kushindwa kutetea hoja kuwa, *usaliti ni sumu ya maendeleo kwa jamii*. Watahiniwa hao walikosa uelewa wa mashairi mbalimbali yaliyopo katika diwani teule ambapo baadhi yao walijadili vipengele vya fani badala ya kutetea hoja kwa kuonesha jinsi wasanii wanavyopinga usaliti katika diwani zao. Wengine walibainisha dhamira mbalimbali kwa hoja kama; *wizi, usaliti, mapenzi*, na *matabaka* kutokana na kutoelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu yasiyo sahihi katika diwani ya "Kimbunga" kwa hoja kama; *tabaka tawala kuwasikiliza tabaka tawaliwa, usawa katika jamii*, *na kupinga/kukataa rushwa*, hoja ambazo ufafanuzi wake haukuwa sahihi. Pia, mtahiniwa mwingine alijadili usaliti katika jamii bila kuhusianisha na diwani walizosoma ambapo alieleza kuhusu "*Usaliti wa Iddi Amini kwa nchi yake.*" Kielelezo Na.13.2 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili kwa kushindwa kukidhi matakwa ya swali.

05. Usaliti ni hali ya kwenda kinyume na makubaliano yaliyopo kati ya watu wawili, jamii na jamii. Usaliti unapotokea kwenye jamii husababisha kurudisha maendeleo katika jamii kutokana na kuharibu nguvu wa vitendea kazi. Wasanii wa diwani wameweza kuonyesha namna au jinsi walivyopinga usaliti katika jamii ili kuweza kuleta maendeleo kwa kutumia diwani ya CHUNGU TAMU iliyoandikwa na THEOBALD. A. MVUNGI pamoja na diwani ya FUNGATE YA UHURU iliyoandikwa na MOHAMED. S. KHATIBU waandishi hawa wameonyesha namna gani walivyopinga usaliti.

Kwa kuanza na diwani ya CHUNGU TAMU iliyoandikwa na THEOBALD A MVUNGI mwandishi ameonyesha namna au njia zifuatazo zilizotumika kupinga usaliti ili kuweza kuleta maendeleo katika jamii

Kuwepo au kuonyesha mapenzi ya kweli na dhati katika mahusiano na ndoa. Ili kuweza kuleta maendeleo katika kujenga jamii kuwa na maendeleo waandishi wameonyesha kuwa ni lazima kuwepo na mapenzi ya kweli au ya dhati kwa watu walio katika mahusiano au ndoa. Kupitia shairi la "Manzese mpaka Ostabei" Mwandishi ameweza kuonyesha umuhimu wa mapenzi ya dhati katika mahusiano.

Kuwepo kwa misingi bora ya demokrasia katika uongozi. Mwandishi pia ametuonyesha kuwa ili tuweze kupinga usaliti hatuna budi kuweza kufuata misingi

| | | |
|---|---|---|
| 05 | bora ya demokrasia katika uongozi kwa viongozi ili kuweza kuondoa ubadhirifu wa rasilimali kwa wananchi na kufanya jamii kuweza kuendelea kimaendeleo. kupitia katika shairi la "Daftari Polisi" mwandishi ameweza kuonyesha jambo hilo kwa undani zaidi. | |
| | kutokuwepo kwa migogoro katika ndoa. Ili kuweza kufeta maendeleo kuanzia ngazi ya familia wanandoa hawana budi kuepukana na migogoro ambayo inaweza pelekea wanafamilia kuanza kufanya usaliti na hivyo kupelekea kupungua imani kwa wanandoa na hivyo kuja kuwepo kwa migogoro. Mwandishi kupitia shairi la "Dotto na kulwa" ameweza kuonyesha jambo hilo kwa undani zaidi. | |


**Kielelezo Na.13.2:** Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 5

Katika Kielelezo Na. 13.2, mtahiniwa alionesha namna ya kuepuka matatizo mbalimbali yaliyojitokeza katika diwani alizosoma badala ya kuonesha jinsi wasanii walivyopinga usaliti. Aidha, mtahiniwa huyo alitoa utangulizi mzuri japokuwa hoja alizotoa hazikukidhi matakwa ya swali na hivyo alipata alama hafifu.

### 2.2.2.2 Swali la 6: Uhakiki wa Ushairi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, katika mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi*. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa mifano dhahiri jinsi kipengele cha mtindo kinavyotofautisha kazi za washairi katika kutoa ujumbe wa kazi zao. kwa kutumia hoja tatu kwa kitabu katika diwani mbili alizosoma.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 29,183 sawa na asilimia 100 ya wote waliofanya mtihani huu. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 26,926 sawa na asilimia 92.27 walipata alama kuanzia 7 hadi 20 kama inavyoonekana katika Chati Na. 11.




**Chati Na. 11:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Katika Chati Na. 11, watahiniwa 2,257 (7.73%) walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5, watahiniwa 4,248 (14.56%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5 na watahiniwa 22,678 (77.71%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 12 hadi 20.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wengi (77.71%) walijibu vizuri swali hili na kupata alama kuanzia alama 12 hadi 20. Watahiniwa hao walionesha umahiri wa kiwango cha juu ambapo kati yao asilimia 26.92 walikuwa na ufaulu mzuri zaidi kwa kupata alama kuanzia 18 hadi 20. Majibu mazuri ya watahiniwa hao yalitokana na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kipengele cha mtindo ambacho hutumika kutofautisha kazi za washairi katika kutoa ujumbe wa kazi zao katika diwani teule. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hilo waliweza kufafanua kwa usahihi hoja tatu kwa kila diwani wakionesha jinsi kipengele cha mtindo kilivyotumika kutofautisha ujumbe wa wasanii katika diwani mbili walizosoma. Baadhi yao walieleza kwa usahihi huku wakitoa mifano dhahiri jinsi kipengele cha mtindo kinavyotofautisha kazi za washairi katika kutoa ujumbe wa kazi zao kwa hoja kama vile *matumizi ya mbinu ya masimulizi*, *matumizi ya picha zinazowiana na ujumbe*, na *mbinu ya kimapokeo na za kimamboleo* kutoka katika diwani ya "Chungu Tamu." Pia katika diwani ya "Fungate ya Uhuru" walieleza mtindo kwa kutoa hoja kama; *mtindo wa msisitizo wima, mtindo wa kidato*, na *mtindo wa nafsi*.

Watahiniwa hao waliweza kueleza mitindo hiyo huku wakitoa mifano dhahiri kutoka katika diwani mbili walizosoma. Kielelezo Na.14.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

6 Mtindo ni namna au jinsi kazi ya fasihi inavyowasilishwa. Mtindo wa uwasilishaji wa kazi ya fasihi humtofautisha mwandishi mmoja na mwandishi mwingine. Kwa kuhusu diwani ya FUNGATE YA UHURU iliyoandikwa na Mohamed S. na KIMBUNGA iliyoandikwa na Haji Gora waandishi hawa wametumia mitindo mbalimbali ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Kwa kuanza na KIMBUNGA zifuatazo ni hoja zinazoonesha mitindo na namna hiyo ya ujumbe;

Mtindo wa kidato, huu ni mtindo wa kuandika ubeti wa shairi ambapo mstari wa mwisho huwa ni nusu katika ubeti huo mwandishi ametoa ujumbe unaosema uongozi mbaya unakuwa wa kupigwa vita kwa kufanya mapinduzi katika ubeti unaoonesha kutokana na uongozi mbaya wananchi wameamua kufanya mapinduzi. Mwandishi anasema

"Kimbunga mji wa siyu, ulichowahi kupiga
Si kwa vule wala huyu, ilikuwa patashika
mibuyu kung'oka minazi kunusuka
nyoyo zilipodhaika"

huo mstari unaosema nyoyo zilipodhaika ndio unaoonesha mtindo wa kidatu.

Mtindo wa nafsi, huu ni mtindo wa kuwasilisha kazi ya fasihi kwa kutumia nafsi hiyo kupitia mtindo huu mwandishi ametoa ujumbe unaosema Uzalendo ni chanzo cha maendeleo katika nchi mpino mwandishi anasema

"Naipenda nchi yangu
naipenda ntakufa naipenda"

6 huyo hata katika jamii hakuna uzalendo ndio cha
nzo cha maendeleo katika nchi.
Mtindo wa kimapokeo, huu ni mtindo wa
mashairi ambao hufuata urari wa vina na mi
zani katika kuwasilisha kupitia mtindo huu
mwandishi ameweza kubeba ujumbe unaose
ma wizi wa mali za umma ni kikwazo
cha maendeleo ya jamii mwandishi ameo
nesha hili kupitia shairi la paka anapose
ma
"Paka nakuwaza wezi, wacha kula samaki
Imekuwa yako kazi, mauzoni kuendeza"
huyo mwandishi anaiasa jamii hasa viongozi
kuacha kula mali za umma ili kumaletea
maendeleo ya jamii. Kwa kumalizia na FUNA
TE YA UHURU zinatokeza ni hoja zinazoonesha
jinsi mtindo ulivyotoa ujumbe
Mtindo wa kubeti, huu ni mtindo ambao
o unahusu kuuliza swali mwandishi ametumia
mtindo huu katika shairi la Si wewe ambapo
ameeleza ujumbe unaosema mapenzi ya uongo ni
chanzo cha migogoro katika jamii hii inathi
bitishwa anaposema
"Si wewe
Ulonitia kwa kweli kuamua kuwabali
nikakanywesha zuwa la mahaba"
huyo mwandishi anaonesha kuwa ili kuwa
na amani na kuepuka migogoro ni lazima
kuwepo na upendo wa kweli.
Mtindo wa kisasa, katika mashairi mo
ngi ya Fungate mwandishi ametumia mtindo
usiofuata urari wa vina na mizani ambapo

6 Kupitia mtindo huu mwandishi ametoa ujumbe mfano katika shairi la Wizi umo mwandishi ametoa ujumbe unaosema wizi ni kikwazo cha maendeleo kwani unarudisha, wizi katika maeneo mbalimbali kama kanisani, hekaluni hata misikitini. Mwandishi anasema

“Wizi umo
kanisani
Msikitini
wanyang'anywao ni waumini”

hivyo mwandishi anawaasa jamii kuwa na uaminifu kwa kuwa ukosefu wa uaminifu umepelekea tatizo la wizi.

Mtindo wa nafsi, mtindo huu umetumika kuonesha watawala ambao baada ya kupata madaraka, huwasahau wananchi wao ambapo mwandishi anatoa ujumbe unaosema uongozi mbaya ni chanzo cha matatizo katika jamii. mwandishi anasema

“Wapiganao
Sio watawalao
Ila hutawaliwa”

hivyo ni kweli kwamba hata jamii ya sasa uongozi mbaya ndio unapelekea matatizo

Hivyo: Basi katika uwasilishaji wa kazi ya fasihi ni muhimu kuzingatia mtindo wa uwasilisha kwani ndio husaidia kupitisha maudhui yaliyokusudiwa kwa jamii husika kama vile mafunzo, maadili, dhamira na ujumbe.

**Kielelezo Na. 14.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 6

Katika Kielelezo Na. 14.1, mtahiniwa alionesha kwa usahihi namna kipengele cha mtindo kinavyotofautisha kazi za wasanii katika kufikisha ujumbe wa kazi zao kwa kubainisha mitindo mbalimbali iliyotumika katika diwani ya “Fungate ya Uhuru” na “Kimbunga”. Aidha, mtahiniwa huyo alinukuu kwa usahihi beti za mashairi yenye mitindo anuwai na ujumbe unaowasilishwa kama mfano.

Watahiniwa 4,248 sawa na asilimia 14.56 waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5. Ufaulu huo ulisababishwa na baadhi ya watahiniwa kubainisha baadhi ya mitindo kwa usahihi lakini wakashindwa kutoa ufafanuzi unaojitosheleza katika kueleza namna ilivyotumika kutofautisha ujumbe wa wasanii katika diwani teule. Majibu ya watahiniwa hao yalikuwa na mapungufu madogo kama vile: kutoa hoja chache, kuchanganya dhana ya muundo na mtindo na kutoa mifano ya miundo badala ya *mtindo* kama swali lilivyomtaka. Pia, baadhi ya watahiniwa walikuwa na mapungufu kwenye nukuu za mashairi. Wengi wao, walinukuu beti ambazo hazikukamilika au baadhi ya maneno hayakunukuliwa kwa usahihi hivyo, kupata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa wengine (2,257) sawa na asilimia 7.73 walikuwa na ufaulu hafifu wa alama kuanzia 0 hadi 6.5. Watahiniwa hao walishindwa kuonesha jinsi mitindo ilivyotumika kubeba ujumbe wa wasanii katika diwani teule. Baadhi ya watahiniwa walijadili dhamira mbalimbali katika diwani hizo kwa hoja kama; *kujitoa mhanga, kupinga suala la matabaka na ubaguzi wa rangi na kupinga uongozi mbaya* kutoka diwani ya "Chungu Tamu" kinyume na matakwa ya swali. Wengine walieleza vipengele vingine vya fani katika diwani hizo kwa hoja kama; *matumizi ya lugha, mtindo, wahusika* na *mandhari* kinyume na matakwa ya swali. Kutokana na kukosa umahiri huo, wapo watahiniwa walioeleza mitindo ya mashairi isiyo sahihi. Kwa mfano mtahiniwa mmoja katika diwani ya "Kimbunga" alieleza mitindo ifuatayo: *mtindo wa* amri, *mtindo wa kuonya*; na katika diwani ya "Chungu Tamu" alitoa hoja kama *mtindo wa tenzi* ambao si mtindo sahihi katika mitindo ya wasanii wa diwani teule, hivyo alipata alama hafifu. Watahiniwa hao walitakiwa kubainisha mitindo mbalimbali iliyotumika kubeba ujumbe wa wasanii katika diwani teule kwa hoja kama: *matumizi ya mbinu za masimulizi, wahusika, picha, nafsi, monolojia/dayalojia, kidato, msisitizo wima na kiitikio/kibwagizo*; mitindo ambayo imetumiwa na wasanii ili kutofautisha ujumbe katika kazi zao. Kielelezo Na.14.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili na kupata alama hafifu.

6. Mtindo; Ni mbinu anayoitumia msanii ili kutofautisha kazi yake na ya wasanii wengine na mbinu hizo hutumika katika kufikisha ujumbe kwa jamii inayohusika. Kwa kutumia diwani ya "CHUNGU TAMU" iliyoandikwa na "THEOBALD A. MVUNGI pamoja na FUNGATE YA UHURU iliyoandikwa na "MOHAMED S. KHATIBU" waandishi hawa wametumia mitindo mbalimbali katika kufikisha ujumbe.

Kwakuanza na diwani ya "CHUNGU TAMU" iliyoandikwa na "THEOBALD MVUNGI" ifuatayo ni mitindo iliyotumika kumtofautisha na wasanii wengine:-

Mtindo wa sabilia; Huu ni mtindo ambao mwandishi anatumia ili kufikisha ujumbe na mtindo huu unakuwa na mistari sita na kuendelea kwa mfano katika shairi la "wimbo wako hotubani" ~~mst~~ msanii anasema:-

"Cheo ki mkononi,
Agizo li mdomoni,
Kila siku yu pembeni,
Mchana kulitwa ndotoni,
Wimbo wake hotubani,
Raia kazi jangweni,"

Mtindo wa tarbia; Huu ni mtindo ambao mashairi yanakuwa na mistari minne; ambapo msanii ametumia mtindo huu katika shairi la "Tishio la binadamu" msanii anasema:-

"Sasa mgomo baridi, Mgomo usokaidi,
Mgomo ulokaidi, Wenye kuweka mpumo,
Dunia nzima, Yatisha, bara na baharini,
Vita vikuu vya mkia ---- "

hivyo msanii katumia mtindo huo kufikisha ujumbe kuwa ni muhimu kuwepo kwa demokrasia ya kweli.

Mtindo wa tamolitha; Msanii ametumia mtindo huu kwa kuonyesha katika shairi la "Chatu na Kuku" msanii anasema:-

"Kuku ataga mayai
Chatu yake ayataka,
Chatu kuku akimkuta,
Chatu panya anamkoonyeza,
Chatu apata kitoweo."


**Kielelezo Na.14.2:** Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 6

Katika Kielelezo Na.14.2, mtahiniwa alifafanua kimakosa aina za miundo ya mashairi katika diwani ya "Chungu Tamu" kama vile *sabilia, tarbia* na *tamelitha* badala ya kueleza kwa mifano dhahiri jinsi kipengele cha mtindo kinavyotofautisha kazi za washairi katika kutoa ujumbe wa kazi zao ambapo hakutumia mifano yoyote kutoka katika diwani teule na hivyo, alipata alama 0.

#### 2.2.2.3 Swali la 7: Uhakiki wa Riwaya

Swali lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, mada ndogo ya *Uhakiki wa Riwaya*. Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kuchambua kasoro za wahusika wakuu katika riwaya teule na lilimtaka mtahiniwa kufafanua kauli; "Hakuna kizuri kisichokuwa na kasoro" kwa kutumia hoja mbili za uzuri na hoja mbili za kasoro za mhusika mkuu mmoja kwa kila kitabu katika riwaya mbili alizosoma.

Watahiniwa 28,195 sawa na asilimia 96.6 walijibu swali hili. Swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri zaidi kwa sababu watahiniwa 28,128 sawa na asilimia 99.76 walipata alama kuanzia 6.5 hadi 20. Chati Na.12 inaonesha viwango vya ufaulu kwa watahiniwa kiasilimia.




**Chati Na.12:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7*

Katika Chati Na. 12, watahiniwa 67 (0.24%) walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5, watahiniwa 575 (2.04%) walifaulu kwa

kiwango cha wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5 na watahiniwa 27,553 (97.72%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 12 hadi 20.

Jumla ya watahiniwa 27,553, sawa na asilimia 97.72 walijibu vizuri swali hili na kupata alama kuanzia 12 hadi 20. Ufaulu mzuri katika swali hili ulitokana na watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya *Uhakiki wa Riwaya*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu wasifu wa wahusika wakuu katika riwaya teule hivyo, kufafanua kwa usahihi hoja zilizoonesha uzuri na kasoro za wahusika hao na hivyo kupata alama za juu katika swali hili. Kati yao, asilimia 74.50 walijibu swali hili vizuri zaidi na kupata alama kuanzia 16 hadi 20. Watahiniwa hao waliweza kufafanua uzuri na kasoro za wahusika mbalimbali. Kwa mfano, *Gaddi Bullah* kutoka katika riwaya ya "Mfadhili" anatumika kama mhusika mwenye kuonesha mapenzi ya dhati, mchangamfu na mchapakazi (uzuri), mwenye kuendekeza mapenzi kunakoathiri utendaji wake wa kazi, mwenye ghadhabu na anayependa asikopendwa (kasoro). Kwa upande wa riwaya ya "Usiku Utakapokwisha", *Gonza* ni mhusika mwenye bidii katika kazi na mhitimu wa elimu ya sekondari (uzuri), anajihusisha na ujambazi uliosababisha kifo chake na mshauri mbaya wa Chioko kuhusu kumtoa dada yake Nelli kama hongo ili waweze kupata kazi (kasoro). Vivyo hivyo, katika riwaya ya "Vuta N'kuvute" walimwonesha mhusika *Jasmin* kuwa ni mwanamke jasiri aliyeamua kuishi maisha magumu ya uswahilini licha ya kutoka katika jamii bora za kihindi, mwenye mapenzi ya dhati kwa Denge na anayependa kujichagulia mchumba anayempenda (uzuri), mwenye kupenda asikopendeka na asiyezingatia taratibu za talaka (kasoro). Aidha, katika riwaya ya "Kufikirika" *Mfalme* ni kiongozi shupavu anayewaunganisha watu na anawanusuru watu wake dhidi ya kafara (uzuri) asiye na maarifa kuhusu utasa wa Malkia na hivyo kuwachosha watu wake katika kutafuta tiba ya Malkia (kasoro). Kielelezo Na. 15.1 kinaonesha sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa katika swali hili.


7. Muhusika mkuu : Ni muhusika anaye onekana kutoka mwanzo na hata mwisho wa Masimulizi ya riwaya au tamthiliya Kwa kutumia riwaya ya "MFADHILI" iliyo andikwa na "HUSSEIN TUWA" na riwaya "VUTA N'KUVUTE" iliyoandikwa na "SHAFI ADAM SHAFI" Mwandishi ameonesha sifa mbaya ya Muhusika mkuu na sifa nzuri ya Muhusika Mkuu kwaku anza na riwaya ya "Mfadhili"

Gaddi Bullah : Ni Muhusika Mkuu aliyejitokeza kutoka mwanzo hadi mwisho wa tamthiliya hii zifuatazo ni sifa nzuri ya Muhusika Gaddi

Ni mtu mwenye upendo wa dhati Gaddi bulla alikuwa mwenye upendo wa dhati hasa kwa Mkewe nyambuja na Dania pamoja na Mtoto wa Dania aitwaye Johnior hivyo ameoneshwa kuwa na upendo

Mchapa kazi : Gaddi bulla ni mtu mwenye ufanisi mkubwa wa kazi na hata amependwa sana na wafanya kazi wenzake pamoja na wakuu wa kazi aliyokuwa akifanya. Pamoja na kuwa na sifa nzuri zifuatazo ni sifa mbaya aliyonayo Gaddi

Aliyumbishwa na Mapenzi : Gaddi alikuwa akiyumbishwa na Mapenzi ya Nyambuja hatimaye kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa na kuhamishwa kituo


7 Alikuwa si mvumilivu: Gaddi
bulla alikuwa si mvumilivu kwani aliishia
dwa kuvumilia Maumivu aliyokuwa
akipata baada ya kuachwa na wapenzi
wake Dania na Nyambuja akashindwa
kufanya kazi kwa ufanisi
kwa kumalizia na riwaya ya "Vuta
n'kuvute"
Yasmini: Ni msichana wa kihindi
aliyeweza kuwepo katika hadidhi kutoka
mwanzo hadi mwisho wa hadithi zifuat
azo ni sifa nzuri ya yasmini
Ni mwanamapinduzi: Yasmini
alikuwa mwanamapinduzi baada ya kuk
ataa kuchaguliwa mchumba na wazazi
wake na kukimbia kwa rafiki yake
Mwajuma hivyo amekuwa msichana
aliyeweza kuwa kioo cha jamii yake
si lazima wazazi kuchagua mtu wa
kuishi nae.
Ni mtu mwenye upendo wa kweli
Yasmini alikuwa na upendo wa kweli kwa
mwajuma pale alipokuwa akikaa nae
kwa upendo katika hali ya umaskini
walionao na Mapungufu walionao.
Kisichokuwa na Madhaifu hakupakamilika
zifuatazo ni sifa mbaya za yasmini
Ni mtu mwenye wanaume wengi
Yasmini alikuwa na wanaume wengi hivyo
alione kama Mwanamke Malaya na haku
weza kuwa na Malengo na Mwanaume
yeyote kama vile Bukheti, Shihabu

**Kielelezo Na. 15.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 7.

Katika Kielelezo Na. 15.1, mtahiniwa aliweza kufafanua uzuri na kasoro za wahusika Gaddi Bullah kutoka katika riwaya ya "Mfadhili" na Jasmin kutoka katika riwaya ya "Vuta N'kuvute" kwa usahihi na hivyo alipata alama za juu.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 575 sawa na asilimia 2.04 ya waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5. Ufaulu wa wastani wa watahiniwa katika kundi hilo ulitokana na baadhi yao kutoa hoja pungufu na wengine walitoa hoja zisizojitosheleza kuhusu uzuri na kasoro za wahusika wakuu katika

riwaya teule katika kutetea kauli kuwa, “hakuna kizuri kisichokuwa na kasoro.” Baadhi ya watahiniwa walielezea wasifu wa ndani na wa nje wa wahusika kama vile; ‘Mfadhili’ (*Gadi Bullah, Dania* na *Jerry*) na “Vuta N’kuvute” (*Denge, Yasmin* na *Mwajuma*) badala ya kufafanua uzuri na kasoro za mhusika mkuu kama swali lilivyotaka, hivyo kupata alama za wastani. Wengine waliweza kuchagua mhusika mkuu mmoja kwa kila riwaya na kufafanua hoja mbili za uzuri na mbili za kasoro za mhusika huyo lakini walitoa ufafanuzi usiojitosheleza, hivyo kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika riwaya zote mbili alizotumia alifafanua upande wa kasoro pekee kuhusu wasifu wa wahusika wakuu bila kufafanua upande wa uzuri kama swali lilivyomtaka. Katika riwaya ya “Vuta N’kuvute” alifafanua kasoro za mhusika mkuu *Yasmin* kama vile *msaliti* na *asiye na mapenzi ya dhati*; na katika riwaya ya “Mfadhili” alifafanua kasoro za mhusika mkuu Gadi Bulla kama mtu mwenye *wivu wa kimapenzi* na *mwenye hasira nyingi,* hivyo alipata alama za wastani.

Hali kadhalika, watahiniwa wachache sana (67) sawa asilimia 0.24 walishindwa kujibu kwa usahihi swali hili. Watahiniwa hao walitumia hoja zisizojitosheleza kuchambua kasoro za mhusika mkuu mmoja kwa kila kitabu katika riwaya mbili walizosoma, hivyo kupata alama hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5. Hii ilitokana na watahiniwa hao kukosa umahiri katika uhakiki wa wasifu wa wahusika wa riwaya teule. Baadhi ya watahiniwa walijadili dhamira zilizoibuliwa na wahusika wakuu katika riwaya teule. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alimtumia mhusika *Gadi Bulla* katika riwaya ya “Mfadhili” aliyeibua dhamira ya *mapenzi ya dhati* na *mchapakazi*; na katika riwaya ya “Usiku Utakapokwisha**”** alimtumia mhusika *Chioko* kuwa aliibua dhamira ya *mapenzi ya dhati kwa mpenzi wake Neli* na *mvumilivu kwenye kutafuta mafanikio.* Kwa ujumla, watahiniwa hao walielewa matakwa ya swali lakini walishindwa kuhusianisha majibu yao na mahitaji ya swali. Wengine walifafanua dhamira zilizojitokeza katika riwaya teule kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijadili dhamira zilizojitokeza katika riwaya teule kama; *uvivu, wizi* na *ulevi* katika riwaya ya “Mama N’tilie” kinyume cha matakwa ya swali. Kielelezo Na.15.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kinyume na matakwa ya swali.

7. Mhusika. ni mtu au kitu chochote ambacho mwandishi ametumia katika kufikisha kazi ya Fasihi kwa Hadhira aliyo ikusudia. Kila muhusika ana Makosa yake na pia ana ~~Ma~~ Mazuri yake kupitia Riwaya mbili ambazo ni MFADHILI na VUTA N'KUVUTE ~~a~~ waandishi wametumika katika kuonesha uzuri na ubaya wa wahusika. Kwa kuanza na Riwaya ya MFADHILI iliyo andikwa na HUSSEIN TUWA ameeleza ubaya na uzuri wa wahusika kama ifuatavyo:

Gaddi Bullah. Huyu ni muhusika Mkuu katika riwaya hii ya Mfadhili ni muhusika ambae ni mwenye Hekima na Busara na anafaa kuigwa katika Jamii kwa baadhi ya mambo kwa mfano Ni mchapa kazi katika Kampuni la Mama mtole, anaupendo kwa watu na wafanyakazi wengine pia anaupendo wa dhati kwa kupenda kazi anayo fanya na anampenda Dania pamoja Nyumbuju. Lakini hafai kuigwa kwa Tabia ya Ulevi na uvutaji wa sigara na kusababisha kampuni kuingia hasara kubwa kutokana na kuachana na mkewe Nyumbuju na kuanza kunywa pombe na kuvuta sigara.

Dania. Huyu ni muhusika mwingine ambae ametumika katika Riwaya hii ili kujenga kazi ya Fasihi. pia muhusika huyu anafaa kuigwa kwa baadhi ya Mambo kwa Mfano ni mchapakazi katika kampuni la Mama mtole ana faa kuigwa kwa uchapakazi wake. Lakini hafai kuigwa kwa baadhi ya Tabia zake kwani ni msaliti kwa kumsaliti Gaddi Bullah baada ya Jerry kuludi Marekani baada ya ufadhili wa Senkuti kumsomesha nje ya nchi Hivyo Gaddi Bullah anaingia kwenye Matatizo mengine na Hatimaye mwishoe alifaliki Gaddi Bullah kwa ugonjwa.

— Bibanuna. Huyu ni ndugu yake wa Damu Gaddi Bullah wanapendana sana hadi kwamba Tatizo la mmoja uapo ni la wote. Anafaa kuigwa kwa Baadhi ya Tabia kwa mfano Bihanuna anaupendo wa kweli upendo huu unajidhihirisha kwanza kwa kaka yake Gaddi bullah pia na ~~B~~ kwa Dania kwa kumuambia lehemu Gaddi Bullah aliko kwa sasa baada ya kumkuta Dania yupo katika hali mbaya (mgonjwa na anahitaji msaada wa ini. Lakini hafai kuigwa kwa Sababu Anajaziba / hasira sana kwa yeyote aliye msaliti kaka yake pia hafai kuigwa kwani Hasikilizi shida za mtu kwa wakati

Kwa kumalizia na Riwaya ya VUTA N'KU
VUTE iliyo andikwa na SHAFI ADAM SHAFI katika
kuelezea Ubaya na uzuri wa wahusika kama ifuatavyo.
Mwajuma. Huyu ni muhusika ambae
muandishi wetu wa Riwaya ya VUTA NKUVUTE Amemtumia
na kuribua suala la ulevi kuwa si zuri. Uzuri wa mhusi
ka huyu ni Ana upendo kwa kila mmoja kwa kumsaidia
Yasmini kumhifadhi ndani kwake pamoja na kumpa
mahitaji yote anayo yataka. Lakini hafai kuigwa ku
tokana na Tabia yake ya ulevi na ameendekeza
kuwa ndiyo starehe yake kila siku jambo litakalo mfa
nya apate umaskini kwani atapunguza juhudi za kufanya
kazi.
Yasmini. Huyu ndiye muhusika mkuu
katika Riwaya yetu ya VUTA N'KUVUTE muandishi
amemuelezea katika uzuri na ubaya wa mhusika Yasmini
Anafaa kuigwa kwa baadhi ya Tabia kwani anaupendo wa
kweli kwa Denge na ni mpambanaji kuhusu Mila na Desturi
zilizo pitwa na wakati kwa kuchaguliwa Bwana wa
kuolewa nae. Pia Hafai kuigwa kwani alimtoroka
Bwana Raza na kwenda kusiko julikana ambapo ni usaliti.
Denge. Huyu ni mpambania uhuru amba
po anapigania uhuru na haki ya Madaraka kwa wakati
ni wa kizungu. Mhusika huyu anafaa kuigwa kwa
ni anamapenzi ya kweli kwa nchi yake kwa kuunda
kundi la kupambania uhuru wa nchi yake. Lakini ha
fai kuigwa kwa sababu Hana Mapenzi ya Dhati kwa
Yasmini angali Yasmini anampenda Denge jambo
linalo pelekea mgogoro kati yake na Yasmini kwa
kukataa kumuoa.
Kwa ujumla. waandishi wa Riwaya
hizi mbili ambapo mwandishi ~~ADAM~~ SHAFI ADAM
SHAFI muandishi wa Riwaya Ya VUTA NKUVUTE ameta
umia kuelezea wahusika Lakini mwandishi mwingi
ne ni HUSSEIN TUWA mwandishi wa Riwaya ya MFA
DHILI amefanikiwa kuwaelezea wahusika hawa
na hivyo kuleta mchango mkubwa katika kuonesha
namna walivyo ibua Dhamira mbalimbali katika
riwaya.


**Kielelezo Na. 15.2:** Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 7.

Katika Kielelezo Na.15.2 mtahiniwa, alieleza wasifu wa wahusika *Gaddi Bullah, Dania* na *Bi Hanuna* katika riwaya ya "Mfadhili" na *Mwajuma, Yasmini na Denge katika riwaya ya* "Vuta N'kuvute" kinyume kabisa na matakwa ya swali, badala ya kutoa hoja mbili za uzuri na hoja mbili za kasoro za mhusika mkuu mmoja kwa kila kitabu katika riwaya mbili teule ili kufafanua kauli "hakuna kizuri kisichokuwa na kasoro."

### 2.2.2.4 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, katika mada ndogo ya *Uhakiki wa Tamthiliya*. Swali lilimtaka mtahiniwa kutathmini umuhimu wa uteuzi mzuri wa mandhari katika kufikisha ujumbe wa kazi za waandishi kwa walengwa kwa kutumia mifano minne kwa kila kitabu katika tamthiliya mbili alizosoma.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 24,535 sawa na asilimia 84.1 ya watahiniwa waliofanya mtihani huu. Kati yao, watahiniwa 24,371 sawa na asilimia 99.33 walifaulu vizuri kwani walipata alama kuanzia 7 hadi 20. Chati Na.12 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na.12:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8*

Katika Chati Na. 12, watahiniwa 164 (0.67%) walikuwa na ufaulu hafifu kuanzia alama 0 hadi 6.5, watahiniwa 1,423 (5.80%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5 na watahiniwa 22,948 (93.53%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 12 hadi 20.

Kulingana na takwimu, swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo watahiniwa wengi (22,948) sawa na asilimia 93.53 walikuwa na ufaulu mzuri kwani walipata alama kuanzia 12 hadi 20. Miongoni mwao, watahiniwa 1,324, sawa na asilimia 26.98 walifaulu vizuri zaidi na kupata alama za juu kuanzia 18 hadi 20. Kwa ujumla, watahiniwa katika kundi hili waliweza kutoa hoja sahihi za kutathmini uteuzi mzuri wa mandhari katika kufikisha ujumbe wa kazi za waandishi kwa walengwa katika tamthiliya mbili alizosoma. Watahiniwa hao walikuwa mahiri katika kuhakiki tamthiliya kwa kubainisha kwa usahihi mandhari yaliyotumika kufikisha ujumbe wa kazi za waandishi wa tamthiliya teule kwa walengwa. Aidha, waliweza kutumia mifano minne kwa kila kitabu kutoka katika tamthiliya mbili walizosoma kama ilivyotakiwa. Kwa mfano, katika tamthiliya ya "Morani" walibainisha *mandhari ya Tanzania miaka ya 1980* yenye kuwasilisha ujumbe wa ulanguzi na uhujumu uchumi, *Ofisini kwa Dongo* (mapambano dhidi ya wahujumu uchumi na kujitoa muhanga), *msituni* (changamoto zinazowapata wapigania haki), na mandhari ya *Sunlight Bar* yenye ujumbe wa ulevi ni kikwazo cha maendeleo. Pia, katika tamthiliya ya "Nguzo Mama" walibainisha mandhari ya *kubuni* yenye ujumbe (umaskini na kunyanyaswa kwa tabaka la chini), mandhari ya *jukwaani* (umoja ni nguvu na utengano ni dhaifu), *mandhari ya ofisini kwa mwenyekiti wa kamati ya mashauri* (uongozi mbaya ni kikwazo cha maendeleo) na mandhari ya *nyumbani kwa Bi Pili na Bwana Sudi* (ulevi ni chanzo cha kutotimiza majukumu ya familia). Kielelezo Na.16.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri swali la 8.

8. Mandhari. Ni mahali au sehemu ambapo kazi ya fasihi imetungwa. Ujenzi mzuri wa mandhari ndio huweza kuibua dhamira na ujumbe au mafunzo mbalimbali ndani ya kazi ya fasihi. Tamthiliya mbili zimeonesha vizuri mandhari hayo na hivyo kuweza kuibua mafunzo na ujumbe mbalimbali. Tamthiliya hizo ni tamthiliya ya MORANI iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo na tamthiliya ya KIVULI KINAISHI iliyoandikwa na Said Mohamed. Kwa kuanza na tamthiliya ya MORANI mwandishi ametumia mazingira mbalimbali na kuibua ujumbe mbalimbali, mandhari hayo ni kama ifuatavyo:-

Mandhari ya Msituni;

Msituni ni sehemu au mahali padipokusanyika miti na uoto mbalimbali wa kupandwa au wa asili. Mwandishi katika mandhari haya amewatumia Wahusika Malongo, mapoto na Mzee waliokuwa wakitafuta nguzo ya Usweri. Ujumbe Umoja na mshikamano ni chachu ya maendeleo kwa jamii.

Mandhari ya nyumbani; Nyumbani ni sehemu ambapo watu huishi au kukaa. Kwa ufupi ni makazi ya watu. Mwandishi ametumia mazingira ya nyumbani kwa Mangimungu. Nyumbani hapo kulikuka mgogoro kati ya Jalia na Mungu chanzo ni Uhujumu uchumi na kujitoa muhanga kwa Jalia. Ujumbe ni Uzalendo na kujitoa muhanga ni njia muhimu ya ujenzi wa jamii mpya.

Mandhari ya mahakamani: Mahakamani

8 kufolewa. Mahakamani katika tamthiliya hii ikiwa na kesi kati ya Mungumungu na Kundi la wanaopinga Uhujumu uchumi, ambapo kesi hiyo ilikukumiwa kwa kuamriwa na rushwa. Ujumbe, rushwa, unyanyasaji na dhuluma ni Chanzo cha Kurudisha nyuma maendeleo ya jamii.

Mandhari ya Klabuni: Klabuni ni mahali ambapo watu hukiza, Kununu na Kunywa pombe na kutumia vilevi vya aina zote. Mwandishi ametumia mandhari ya Klabuni Kuibua dhamira ya ulevi. Mwandishi amemtumia mhusika Aisha na yusuf ambao wanatumia Sigara aina ya Rex. Ujumbe, Ulevi ni adui wa maendeleo na ujenzi wa jamii mpya.

Pia tamthiliya ya KIVULI KINAISHI mwandishi ametumia mandhari kuibua ujumbe mbalimbali. Mandhari hayo ni kama ifuatavyo:-

Mandhari ya nyumbani: Mwandishi ametumia mandhari ya nyumbani Kwa Bi Kizee. Mwandishi anamuonesha Bi Kizee akiwasimulia watoto juu ya uovu, unaoendelea Giningi. Pia mwandishi anamuonesha Bi. kizee akiwapaka watoto dawa. Hivyo, Ujumbe ni malezi bora ya watoto ni chanzo cha kujenga Jamii mpya. Kwa ni simulizi ya Bi Kizee inawafanya watoto kuelewa juu ya uovu unaoendelea Giningi. Na hivyo kuwa tayari kupambana na mbinu hiyo.

Mandhari ya getini: Getini ni Sehemu ya Mlango ya ugo uliozunguka nyumba au eneo fulani. Katika tamthiliya hii mwandishi ameonesha mandhari haya kwa kumtumia mhu-

8 utika Jawabu II ambaye alipokea rushwa kutoka kwa Mfanyabiashara na Mtolewa. Hivyo mwandishi katika mandhari haya ameonesha na kuibua dhamira ya rushwa. Ujumbe rushwa ni adui wa haki hivyo hatuna budi kuing'oa.

Mandhari ya Giningi; Giningi ni eneo la kufikirika au nchi ambayo ndani yake imetawaliwa na viongozi wanafiki, wabinafsi, wachawi. Giningi katika tamthiliya hii imewakilishwa zaidi na Bi Kirembwe, ambaye yeye ni kiongozi mwongo, mchawi, mnafiki. Hivyo Giningi imeibua dhamira ya uongozi mbaya. Ujumbe. Uongozi mbaya ni chanzo cha kuharibu na kurudisha nyuma maendeleo ya jamii hivyo hauna budi kung'olewa.

Mandhari ya jukwaani; Jukwaani ni mahali au sehemu ambapo kazi ya fasihi katika tamthiliya hutendeka. Katika tamthiliya hii jukwaani pameibua dhamira ya mauaji ya wanyonge, mabavu na ubinafsi wa madaraka Bi. Kirembwe aliwaua Mtolewa, Ngari, pamoja na wale wazee na watangazaji. Hivyo, Ujumbe, Mauaji siyo suluhisho la matatizo kwani hata Bi. Kirembwe aliwaua lakini hakutatua tatizo.

Hivyo basi, mwandishi yeyote yule wa tamthiliya wa tamthiliya ni lazima awe na ufahamu na afanye uteuzi mzuri wa mandhari. Kwani uteuzi bora wa mandhari ndio nyenzo na njia muhimu sana katika kuibua dhamira, migogoro, na ujumbe ndani ya kazi ya fasihi.

**Kielelezo Na. 16.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 8.

Katika Kielelezo Na. 16.1, mtahiniwa alithibitisha kwa usahihi jinsi uteuzi mzuri wa mandhari hufikisha ujumbe wa kazi za waandishi kwa walengwa kwa kutumia mifano minne kwa kila kitabu kutoka tamthiliya ya "Morani" na "Kivuli Kinaishi." Vilevile, mtahiniwa

alieleza vizuri maana ya mandhari na aliandika utangulizi na hitimisho zuri linaloendena na swali na kupata alama za juu.

Vilevile, watahiniwa 1,423 sawa na asilimia 5.80 walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uteuzi mzuri wa mandhari katika kufikisha ujumbe wa kazi za waandishi kwa walengwa katika tamthiliya teule. Kutokana na kukosa weledi huo, baadhi ya watahiniwa waliandika utangulizi na hitimisho lisiloendana na swali na walijadili hoja bila kutumia mifano dhahiri ya mandhari na ujumbe stahiki kutoka katika tamthiliya teule. Watahiniwa wengine walibainisha mandhari zinavyojitokeza katika tamthiliya teule bila kuelezea umuhimu wake katika kufikisha ujumbe wa kazi za waandishi kwa walengwa, hivyo walipata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa wachache (164) sawa na asilimia 0.67 waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo kuhusu uteuzi mzuri wa mandhari katika kufikisha ujumbe wa kazi za waandishi kwa walengwa katika tamthiliya teule. Baadhi ya watahiniwa walitoa hoja zisizo sahihi katika kuonesha jinsi uteuzi mzuri wa mandhari unavyofikisha ujumbe katika tamthiliya teule. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika tamthiliya ya "Morani"alitoa hoja kama vile *huchochea ushirikiano, huchochea maendeleo na ujasiri, hukosoa jamii* na *huelimisha jamii*. Katika tamthiliya ya "Nguzo Mama" mtahiniwa huyo alitoa hoja kama vile *husaidia kuchochea maendeleo, huelimisha jamii, hujenga ushirikiano*, *na huburudisha jamii*; bila kuhusisha mandhari ambayo ndiyo msingi wa swali hili. Watahiniwa wengine walioshindwa kujibu swali hili walijadili dhamira mbalimbali katika tamthiliya teule. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika tamthiliya ya "Kivuli Kinaishi" alitoa hoja kama; *rushwa, matabaka* na *imani za kishirikina.* Katika tamthiliya ya "Kwenye Ukingo wa Thim"; alibainisha hoja za *mila potofu katika jamii, malezi mabaya* na *uongozi mbaya*. Pia katika tamthiliya ya "Nguzo Mama" alijadili dhamira za *kupiga vita usaliti*, *migogoro*, *nafasi ya mwanamke katika jamii*, na *kupiga vita rushwa* bila kuhusisha matumizi ya mandhari yaliyotumika kuzalisha dhamira hizo, hivyo alikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Kielelezo Na.16.2 ni sampuli ya sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.

Uteuzi mzuri wa mandhari, husaidia kupata falsafa nzuri ya Mwandishi; Mwandishi kupitia sehemu nzuri ya mazingira huweza kupata falsafa nzuri ya kimapinduzi na kifani kufikisha ujumbe kama fani hayo mzunguka kama kumalizia na tamthiliya ya "Nguzo mama" kama ifuatavyo.

Uteuzi mzuri wa mandhari hupeleka kwa msanii kuibua dhamira; Mwandishi "Penina Muhando" Anatumia mandhari halisia ya Tanzania (nchi ya Tanzania) katika kuonyesha dhamira ya umoja wa wanawake katika kupigania haki zao za msingi. Mfano tunaona Bi nne na Bi moza, Bi pili na wengine pamoja na Bi nane mwenyekiti wao wa kijiji cha patata wanavyo pambana na kuinua nguzo. Hivyo anasawili na maisha asilia ya watanzania.

Uteuzi Mzuri wa mandhari, husaidia kuibua dhamira ya uhalifu. Mwandishi anatumia mandhari alipotoa ukweli juu ya uongozi mbaya wa Bi nane, kama kukosa ukosefu wa vifaa vya shule kama vitabu vya masomo ya sayansi; Hivyo kupitia uteuzi mzuri wa mandhari husaidia msanii kuunda dhamira.

Uteuzi mzuri wa mandhari hupeleka kuibua dhamira ya dhuluma; katika tamthiliya ya "Nguzo mama", Mwandishi "Penina Muhando" anaonyesha dhuluma kwa kumtumia mhusika Bi saba, pale tu baada ya kifo cha mume wake shemeji zake walichukua mali zote na watoto wake na kumwacha anateseka tu. Hivyo mwandishi anasawili na maisha halisi ya watanzania.

**Kielelezo Na.16.2:** Sehemu ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 8

Katika Kielelezo Na. 16.2, mtahiniwa alieleza sababu za uteuzi wa mandhari katika tamthiliya ya "Nguzo Mama" kinyume cha matakwa ya swali badala ya kuonesha jinsi mandhari zinavyofanikisha kufikisha ujumbe wa kazi za waandishi kwa walengwa.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA MADA

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa somo la Kiswahili unaonesha kuwa, watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri katika mada zote (12) zilizotahiniwa. Ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2023 umeongezeka katika mada sita ikilinganishwa na mwaka 2022. Mada zilizoongezeka ufaulu ni pamoja na: *Riwaya* (99.76%), *Maendeleo ya Kiswahili* (99.47%), *Tamthiliya* (99.33%), *Usanifu wa Maandishi* (95.43%), *Matumizi ya Sarufi* (77.91%) na *Tafsiri na Ukalimani* (60.77%). Ongezeko la ufaulu katika mada hizo ulikuwa wa asilimia 0.25, 0.75, 14.63, 41.88, 14.48 na 16.69 mtawalia. Ongezeko kubwa la asilimia 41.88 la ufaulu katika mada ya *Usanifu wa Maandishi* linadhihirisha jitihada kubwa zilizofanyika katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada hii iliyokuwa na kiwango cha chini cha ufaulu kwa mwaka uliotangulia. Pia, mada ya *Maendeleo ya Fasihi Simulizi* iliyotahiniwa mwaka 2023 ilikuwa na ufaulu mzuri wa asilimia 92.15.

Kwa upande mwingine, ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2023 umepungua katika mada tano (5) ikilinganishwa na mwaka 2022. Mada zilizopungua kiwango cha ufaulu ni *Utumizi wa Lugha* (97.92), *Ushairi* (90.96%), *Utungaji* (89.92%), *Ufahamu na Ufupisho* (85.60%), na *Fasihi kwa Ujumla* (70.54%). Upungufu wa ufaulu kwa mada hizo ni asilimia 0.4, 7.23, 10, 9.09 na 16.76 mtawalia. Kiwango cha kushuka kwa ufaulu mwaka 2023 ikilinganishwa na mwaka 2022 kilitofautiana kati ya mada moja na nyingine ambapo mada ya *Fasihi kwa Ujumla* ilishuka kwa kiwango kikubwa cha asilimia 16.76 ikifuatiwa na mada ya *Utungaji* iliyoshuka kwa asilimia 10. Hata hivyo, mada za *Utumizi wa Lugha, Ushairi*, na *Ufahamu na Ufupisho* zilikuwa na mwachano mdogo wa asilimia 0.4, 7.23, na 9.09 mtawalia.

Licha ya mada ya *Tafsiri na Ukalimani* kuwa na matokeo ya chini zaidi (60.77) kwa mwaka 2023, kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika mada zote ulikuwa mzuri sawa na mwaka 2022 ambapo, asilimia 100 ya watahiniwa walipata alama zaidi ya 35 katika mada zote. Hii inadhihirisha kuwa, watahiniwa walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu mada nyingi zilizotahiniwa ukihusisha uelewa wa dhana za kifasihi na kisarufi, matumizi sahihi ya lugha, uzingatiaji wa alama za uandishi, uhakiki wa kazi za kifasihi, ufahamu na usanifu wa maandishi ya kifasihi huku wakitoa hoja sahihi zenye mifano thabiti.

## 4.0 HITIMISHO

Taarifa hii inaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika mtihani wa *121 Kiswahili* kwa mwaka 2023 kilikuwa kizuri kwani asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walifaulu. Ufaulu katika mada zote (12) ulikuwa mzuri ambapo wastani wa ufaulu ulikuwa ni asilimia 88.31. Ufaulu mzuri umetokana na watahiniwa kuwa na maarifa, ujuzi na weledi wa mada mbalimbali zilizotahiniwa. Kiwango hiki cha ufaulu wa watahiniwa ni cha juu zaidi kwa asilimia 4.67 ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu wa mada cha mwaka 2022 ambapo wastani wa ufaulu wa mada zote ulikuwa asilimia 83.64.

Uchambuzi uliofanyika unaonesha kuwa watahiniwa walifanya vizuri katika mtihani wa somo hili kutokana na sababu kama vile *kuzingatia matakwa ya swali, uelewa mkubwa wa mada kuu na mada ndogo, uwezo mkubwa katika kujibu maswali* na *kutetea au kuthibitisha hoja kwa kutumia mifano.* Hata hivyo, mada ya *Tafsiri na Ukalimani* ilikuwa na ufaulu mzuri japokuwa ilikuwa na matokeo ya chini zaidi kutokana na kuwa na majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya vipengele vya tafsiri.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ufaulu wa somo la 121 Kiswahili ni mzuri kutokana na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali na wadau wengine wa elimu. Hata hivyo, ili kuinua kiwango cha ufaulu katika mada ya *Tafsiri na Ukalimani* yafuatayo yanashauriwa kufanyika:

(a) Wanafunzi wasome matini mbalimbali za kifasihi kisha wabaini mbinu mbalimbali za kisanaa zilizotumika katika matini hizo ili wazifanyie mazoezi ya kuzitafsiri kwa kutumia mbinu anuwai za tafsiri.

(b) Walimu wawaongoze wanafunzi kufanya mazoezi ya kutafsiri matini katika mikabala mbalimbali ili kupata ujuzi wa kutumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika miktadha mbalimbali.

(c) Walimu wawaongoze wanafunzi kufanya mazoezi ya kukalimani mazungumzo anuwai ili kupata umahiri wa kutumia mbinu mwafaka katika kutafsiri matini kutoka lugha ya Kiswahili kwenda Kiingereza na Kiingereza kwenda Kiswahili.

**UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2023**

**121 Kiswahili**

| Na. | Mada | Idadi ya Maswali | Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa kwa Mada | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | *Riwaya* | 1 | 99.76 | Vizuri |
| 2. | *Maendeleo ya Lugha* | 2 | 99.47 | Vizuri |
| 3. | *Tamthiliya* | 1 | 99.33 | Vizuri |
| 4. | *Utumizi wa Lugha* | 1 | 97.92 | Vizuri |
| 5. | *Usanifu wa Maandishi* | 1 | 95.43 | Vizuri |
| 6. | *Maendeleo ya Fasihi Simulizi* | 1 | 92.15 | Vizuri |
| 7. | *Ushairi* | 2 | 90.96 | Vizuri |
| 8. | *Utungaji* | 1 | 89.92 | Vizuri |
| 9. | Ufahamu na Ufupisho | 1 | 85.60 | Vizuri |
| 10. | *Matumizi ya Sarufi* | 2 | 77.91 | Vizuri |
| 11. | *Fasihi kwa Ujumla* | 2 | 70.54 | Vizuri |
| 12. | *Tafsiri na Ukalimani* | 1 | 60.77 | Vizuri |

**ULINGANIFU WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MWAKA 2022 NA 2023**

